

LIBERTY SPARKS
For a Freer & Prosperous Society
(THINK TANK)

# MAENDELEO KATIKA UHURU WA KIUCHUMI TANZANIA

## RIPOTI

## 2022

Kwa Hisani ya: FRASER INSTITUTE ATLAS NETWORK

## WANACHAMA WA KIKUNDI KAZI

**IMEANDALIWA NA**

Prof Samuel wangwe
Dr Petro Sauti Magai

**IMELETWA NA**

Liberty Sparks

## Yaliyomo


MUHTASARI MAHSUSI .......... 5

1.0 UTANGULIZI .......... 10

2.0 MALENGO, MITAZAMO NA MBINU .......... 12

2.1 Malengo ya Utafiti .......... 12

2.2 Mwelekeo wa Utafiti .......... 12

2.3 Mbinu za Utafiti .......... 12

3.0 UELEWA ULIOPATIKANA KUPITIA VITABU NA MAANDIKO MBALIMBALI .......... 14

3.1 Uhusiano kati ya Uhuru wa Kiuchumi na Ukuaji wa Kiuchumi (pato la taifa) .......... 14

3.2 Ustawi na Uhuru wa Kiuchumi .......... 19

4.0 MATOKEO YA UTAFITI .......... 23

4.1 Utangulizi .......... 23

4.2 Tanzania 2021 “Kielezi cha Uhuru wa Kiuchumi” katika Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi .......... 25

4.2.1 Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi .......... 27

4.2.2 Uhuru wa Mahakama .......... 29

4.2.3 Uadilifu wa Mfumo wa Kisheria .......... 30

4.2.4 Ulinzi wa Haki ya Kumiliki Ardhi .......... 32

4.2.5 Marekebisho ya sheria za haki kijinsia .......... 33

4.2.6 Haki Jinai na Mahakama Zisizopendelea .......... 35

4.2.7 Utekelezaji wa Mikataba Kisheria .......... 36

4.2.8 Ulinganishi wa Nchi katika Utawala Unaozingatia Sheria na Haki ya Kumiliki Ardhi .......... 37

4.3 Uwezo wa Kuwa na Uimara wa Sarafu .......... 39

4.3.1 Ukuaji wa fedha .......... 40

4.3.2 Mfumuko wa Bei .......... 43

4.3.3 Kiasi kinachokubalika cha Kupanda na Kushuka kwa Mfumuko wa Bei .......... 45

4.3.4 Uhuru wa Kumiliki Akaunti za Benki kwa Fedha za Kigeni .......... 46

4.3.5 Ulinganishi baina ya Tanzania na Nchi zilizochaguliwa katika Uimara wa Sarafu .......... 49

4.4 Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa .......... 51

4.4.1 Kodi kwenye Biashara ya Kimataifa .......... 53

4.4.2 Wastani wa Kiwango cha ushuru .......... 53

4.4.3 Kanuni ya Vikwazo vya Biashara .......... 55

4.4.4 Ulinganishi wa Nchi kwenye Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa .......... 57

4.5 Sheria .......... 59

4.5.1 Udhibiti wa Soko la Mikopo ........ 60
4.5.2 Udhibiti wa Kiwango cha Riba ........ 62
4.5.3 Udhibiti wa Soko la Nguvukazi ........ 64
4.5.4 Udhibiti wa biashara ........ 66
4.5.5 Ulinganishi baina ya Tanzania na Nchi zilizochaguliwa katika Biashara Udhibiti ........ 67
5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 70
5.1 Hitimisho ........ 70
5.2 Mapendekezo ........ 71
REJEA ........ 76

## MUHTASARI MAHSUSI

Utangulizi

Kwa mujibu wa ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021), orodha iliyochapishwa ya Uhuru wa Kiuchumi Duniani inaonesha kiasi ambacho sera na taasisi za nchi husaidia katika kuongeza uhuru wa kiuchumi. Muundo wa kielezo cha uhuru wa kiuchumi duniani unaonesha kiasi cha uhuru wa kiuchumi katika maeneo makuu matano, ambayo ni; Ukubwa wa Serikali; Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi; Uimara wa Sarafu; Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa, na Udhibiti. Manufaa ya kiuchumi yanayoonekana wazi ya uhuru wa kiuchumi yamepelekea uwazi ulioongezeka kwenye biashara na mageuzi mengine yenye mwelekeo wa soko katika nchi zinazoendelea, katika iliyokuwa ngome ya Sovieti ya Ulaya Mashariki, na hata katika nchi zenye uchumi ulioendelea. Kielezi cha ripoti ya uhuru wa kiuchumi kimeiweka Tanzania katika fungu la tatu pamoja na nchi kama vile Kenya, Rwanda, Zambia, Afrika Kusini, Botswana, Nigeria, na Namibia. Katika ripoti hii, Tanzania ilipata kiwango cha 6.75 na kushika nafasi ya 97 kati ya nchi 165. Katika Afrika kusini mwa Sahara, Tanzania inashika nafasi ya nane kati ya nchi 47 na kiwango chake cha jumla kipo juu ya wastani wa eneo hilo, ingawa kipo chini ya wastani wa dunia. Ripoti imesisitiza kwamba uhuru wa kiuchumi has matokeo makubwa katika kutokomeza umaskini na kuboresha ustawi wa Watanzania.

Lengo na Mbinu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchanganua ripoti ya Taasisi ya Fraser iliyotolewa hivi karibuni ya "Orodha ya Nchi kwa Viwango vya Uhuru wa Kiuchumi Duniani", na kufanya uchanganuzi kuchunguza "Kiwango cha Uboreshaji wa Uhuru wa Kiuchumi Tanzania 2021. Utafiti huu umetumia mbinu mchanganyiko za utafiti kufanya zoezi hili. Mbinu ya utafiti ya kupima ubora ilitumika kuchukua taarifa kutoka kwenye nyaraka sahihi na watoa taarifa waliochaguliwa. Katika zoezi hili, aina zote mbili za data; data msingi na data sekondari ziliochukuliwa na kuchanganuliwa. Vyanzo sekondari zilipatikana kimsingi kutoka kwenye uhakiki na uchanganuzi wa Orodha ya Nchi kwa Viwango vya Uhuru wa Kiuchumi Duniani ya mwaka 2021 iliyotolewa na Taasisi ya Fraser. Kwa lengo la utafiti huu, maeneo makuu manne ya uhuru wa kiuchumi yameangaliwa kikamilifu, ambayo ni; Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi, Uimara wa Sarafu, Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa na Udhibiti. Utaratibu uliopelekea kukamilika kwa zoezi unahusisha kufanyika kwa majadiliano na kushirikisha taarifa husika zilizoainishwa kwenye michakato ya utayarishaji wa sera nchini Tanzania na kutoa uboreshaji wa hali ya juu

viwango vya uhuru wa kiuchumi nchini Tanzania na mapendekezo ya sera kwa ajili ya kuwasilishwa kwa watunga sera.

Matokeo Makuu ya Utafiti

(i) Uelewa uliopatikana kupitia umeashiria kwamba uhuru wa kiuchumi hupelekea ukuaji wa kiuchumi na ustawi wa jamii. Hata hivyo, matokeo ya utafiti kuhusu uhusiano chanya baina ya uhuru na ukuaji wa kiuchumi na ustawi wa jamii yanaonesha mapungufu fulani. Maana yake ni kwamba ni sharti kuwe na vigezo vingine vya kuzingatia katika muktadha maalumu.

(ii) Ufanisi wa Tanzania kuhusiana na mfumo wa kisheria na haki ya kumiliki ardhi uliendelea, kwa kiasi fulani, kubakia katika kiwango kilekile huku kiwango cha juu zaidi kikiwa nikikiwa ni 5.57 mwaka 2017 na kiwango cha chini zaidi kikiwa ni 5.3 mwaka 2019. Kiwango cha uhuru wa mahakama kilikuwa 5.29 na 5.4 mwaka 2018 na 2019 mtawalia. Hata hivyo, kulikuwa na kushuka kwa ujumla kwa Tanzania katika mfumo wa kisheria na haki ya kumiliki ardhi. Kushuka huko kwa sehemu fulani kulitokana na marekebisho ya sheria mbalimbali yaliyoshusha haki ya kumiliki ardhi kwa wamiliki wa ardhi. Pia ilipelekea kushuka kwa uhuru katika mfumo wa mahakama, kamapale ambapo serikali kama mihimili wa dola ulitwaa madaraka makubwa na kuipuuza mihimili mingine katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2020. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2020 kulikuwa na kasi ya kushuka kwa hali ya kuheshimu katiba au sheria kama ilivyoonekana kwa kuwafukuza kazi watumishi wa ngazi za juu serikalini katika mikutano ya hadhara kinyume na sheria ya utumishi wa umma na orodha ndefu ya makosa yasiyo na dhamana chini ya Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu iliyotumiwa katika kesi dhidi ya wapinzani wa kisiasa wa serikali na waandishi wa habari wenye kuikosoa serikali.

(iii) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakataza aina zote za ubaguzi. Haki za wanawake zimethibitishwa kikatiba lakini hazilindwi kwa ulinganifu. Licha ya kuwepo kwa sheria hizi za moja kwa moja, ikiwemo sheria mama inayolinda haki za wanawake chini Tanzania, bado kuna changamoto zinazowakabili wanawake. Idadi kubwa kiasi ya wanawake hawana uwezo wa kufanikisha haki yao ya kumiliki ardhi na mali nyingine kutokana na ukosefu wa uelewa wa sheria hizi na changamoto za utekelezaji wake. Kikwazo kikuu cha haki ya wanawake ya kumiliki ardhi ni kuwepo kwa sheria za

mila, mazoea, desturi za urithi, mila na desturi zinazowanyima wanawake haki ya kumiliki mali.

(iv) Kiwango katika uimara wa sarafu kimekuwa kizuri kwa zaidi ya 9.0. Mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi unaridhisha. Dalili ya kudumishwa kwa sera jumuishi ya fedha na kuboresha mazingira ya kufanya biashara. Mfumuko wa bei umekuwa umedhibitiwa kama inavyoonekana katika kiwango chake na kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka.

(v) Mabenki na taasisi za fedha zinaruhusiwa to kutoa huduma ya fedha za kigeni kwa wakazi kuhusiana na malipo yote ya ya ndani na kigeni na jambo hili limebaki katika kiwango cha juu katika kipindi cha 2015-2019 kwa sababu katika kipindi hicho hapakuwa na mabadiliko yoyote katika udhibiti wa Serikali unaohusiana na umiliki na uendeshaji wa akaunti za benki katika fedha za kigeni.

Kumekuwa na kiwango cha chini cha mabadiliko katika uhuru wa kufanya biashara ya kimataifa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2019. Hii ni dalili ya uimara wa sera ya serikali katika kanuni zinazosimamia biashara ya kimataifa. Hata hivyo, kiwango cha mapato yatokanayo na kodi inayotozwa katika biashara kilishuka sana kutoka 8.82 mwaka 2015 hadi 7.34 mwaka 2019. Matokeo ya utafiti yalionesha, Tanzania ilifanya vibaya sana katika usimamizi wa vikwazo vya biashara na udhibiti, kiwango chake kikiwa 2.91 mwaka 2019, ambacho kilikuwa cha chini kuliko wastani

(vi) Vikwazo visivyokuwa vya kifedha (NTBs) katika biashara vilifikia kiwango cha 4.82 mwaka 2016 kikipanda hadi 5.03 mwaka 2019 wakati ambapo gharama za lazima za kuagiza bidhaa/huduma toka nje na kuuza nje bidhaa/huduma zilibaki katika kiwango chake cha 0.80. Soko la biashara za magendo lilibaki katika kiwango chake cha 10.00 kipindi chote cha mwaka husika. Hii ilikuwa vivyohivyo katika uhuru wa wageni kutembelea Tanzania.

(vii) Katika masharti ya mikopo, Tanzania ni ni nchi ya 58. Hii inamaanisha kwamba wafanyabiashara na wajasiriamali wanapitia ugumu usio wa lazima katika kupata mikopo kuanzisha au kutanua biashara na kutengeneza ajira na ustawi. Tanzania ilishika nafasi ya 13 kati ya nchi 15 kutoka Afrika kusimi mwa Sahara katika urahisi wa kupata mikopo. Kama soko linaloibuka, miradi mingi ya kibiashara nchini Tanzania imehangaika na uwezekano mgumu wa kupata mikopo, na asilimia 70 ya biashara zote

za kati na ndogo nchini Tanzania, hazina uwezekano rasmi wa kupata mikopo kabisa. Kwa kweli, ni asilimia 15 tu ya watu wote ndio wenye uwezekano rasmi wa kupata mikopo kupitia mabenki.

(viii) Ukosefu wa mikopo haumaanishi kwamba Watanzania siyo wakopaji wa fedha, kwa kuwa zaidi ya nusu ya wale waliopo katika katika soko la nguvukazi wamewahi kuchukua mikopo wakati fulani. Watanzania wengi wanatumia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi.

(ix) Uchanganuzi wa ufanisi wake kupitia Taasisi ya Fraser umeashiria kwamba, kiwango cha udhibiti wa soko la mikopo mwaka 2017 kilikuwa 7.84, ambapo kiasi hicho kiliongezeka kwa 0.32 mwaka 2018 hadi 8.18, kiwango hicho kilibaki katika ufanisi wake uleule mwaka 2019. Kiwango kinaonekana hivyo kwa sasa. Kufuatia janga la korona, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kuchukua mlolongo wa hatua za kisera kuitegemeza sekta ya kibenki, ikiwemo kushusha kiwangocha cini cha riba kutoka 7.0% hadi 5.0% na kupunguza kiwango cha chini cha uwiano wa mali kutoka 7.0% hadi 6.0% rasmi rasmi kuanzia 8 Juni 2020, ili kuchochea kuimarika kwa ufanisi wa soko. Licha ya mdororo wa dunia katika mikopo ya kifedha na ukuaji mwaka 2020 kutokana na UVIKO-19, sekta ya kibenki nchini Tanzania lilendelea kuimarika katika kiwango chake cha 4.1% kwa mwaka. huduma za kibenki kwa njia ya kidijitali zinaendelea kutanuka zikichochewa na kukua kwa ujumuishwaji wa kiuchumi na kiwango cha kuenea kwa matumizi ya simu za mkononi.

(x) Matokeo ya utafiti kuhusu ufanisi wa udhibiti wa kiwango cha riba (viwango hasi vya riba halisi) kyanaonyesha kwamba Tanzania iliweza kudhibiti riba katika kiwango kisichobadilika kutoka 2015 hadi 2017 kwa ufanisi wa 10 ukiporomoka taratibu hadi 9

(xi) Wakazi wanafurahia kiasi fulani cha uhuru wa msingi unaofungamana na kusafiri na kubadili eneo la makazi, ajira, na elimu hasa wale wanaotoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati ambapo Itifaki ya Soko la Pamoja, inayohusisha uhamishaji huru wa nguvukazi, inatekelezwa ingawa siyo kikamilifu.

Mapendekezo

i. Hapana budi kuchukua hatua ili kufikia viashiria vya msingi vya uhuru wa kiuchumi.

ii. Hali ya kuteleza iliyoonekana katika mwenendo kuhusiana na mfumo wa kisheria na haki ya kumiliki ardhi inastahili kutazamwa kwa umakini kwa kufanya uhakiki wa marekebisho yaliyofanyika katika sheria mbalimbali zilizoshusha haki ya kumiliki ardhi au kupelekea kushuka kwa uhuru katika mfumo wa mahakama.

iii. Haki ya wanawake kumiliki ardhi haina budi kuhimizwa kupitia ukuzaji wa kiwango cha uelewa wa sheria na uimarishaji wa mbinu za utekelezaji.

iv. Vikwazo vya kudhibiti biashara ambavyo vimekuwa vikali zaidi katika miaka mitano iliyopita havina budi kulegezwa.

v. Ongeza kasi ya kufanya usimamizi wa kibenki kwa uangalifu zaidi na kuchochea tasnia madhubuti na kuendelea kutanua huduma za kifedha kwa njia ya mtandao wa simu na intaneti, ujumuishwaji wa kiuchumi na boresha mikopo kutoka sekta binafsi wakati huohuo punguza idadi ya mikopo inayosuasua.

vi.

vii. Udhibiti wa soko la nguvukazi hauna budi kuweka mizania kati ya kuwezesha mazingira bora ya kufanya kazi na vipato kwa waajiriwa.

viii. Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja, inayohusisha uhamishaji huru wa nguvukazi, hauna budi kuharakishwa na maendeleo yake kufanyiwa tathmini kwa kuzingatia uhuru wa msingi unaohusika.

## 1.0 UTANGULIZI

Ripoti ya Uhuru wa Kiuchumi Duniani 2021 inapima kiasi ambacho sera na taasisi za nchi husaidia katika kuongeza uhuru wa kiuchumi. Muundo wa kielezo cha uhuru wa kiuchumi duniani unaonesha kiasi cha uhuru wa kiuchumi unaoonekana katika maeneo makuu matano, ambayo ni; Ukubwa wa Serikali, Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi, Uimara wa Sarafu, Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa, na Udhibiti. Katika orodha, maeneo hayo makuu matano yamegawanyika katika vigezo vikuu 24. Vingi kati ya vigezo vikuu hivi navyo vinaundwa na vigezo vidogo kadhaa. Kwa ujumla, orodha inahusisha vigezo tofauti 42 vinavyobadilika. Kila kigezo kikuu kimepewa kipimo kinachoanzia 0 hadi 10 kinachoakisi mgawanyo wa msingi wa data. Pale vigezo vidogo vinapokuwepo, vinatengeneza wastani unaopelekea kiwango cha kigezo kikuu. Viwango vya kigezo kikuu ndani ya kila eneo vinatengeneza wastani unaopelekea viwango kwa kila eneo miongoni mwa maeneo matano kama ilivyofafanuliwa hapa chini:-

Katika jamii zilizo huru kiuchumi, serikali huwa zinaruhusu nguvukazi, mtaji na bidhaa kuhama bila kizuizi, na hujiepusha na matumizi ya mabavu au vikwazo dhidi ya uhuru wa watu kupita kiasi kinachohitajika kwa ajili ya kulinda na kudumisha uhuru wa watu (ripoti ya Taasisi ya Fraser, 2021). Kwa minajili ya kupata kiwango cha juu cha uhuru wa kiuchumi, nchi inalazimika kutoa ulinzi wa uhakika wa mali za watu binafsi, mfumo wa kisheria unaowapa watu wote haki kwa usawa, utekelezaji wa mikataba bila ubaguzi, na mazingira tulivu kifedha. Pia inalazimika kutoza viwango vya chini vya kodi, kujiepusha na uanzishaji wa vikwazo dhidi ya biashara ya ndani na biashara ya kimataifa, na kutegemea zaidi masoko badala ya matumizi ya serikali na udhibiti katika mgawanyo wa bidhaa na rasilimali (Nikolaev na wenzake, 2017).

Uhuru wa kiuchumi ni dhana inayowakilisha vipengele mbalimbali vya uchumi. Inapima jinsi nchi inavyoathiriana na uchumi wa dunia kama vile katika fikra zinazopendelea mabadiliko ya kifedha, uhuru wa kufanya biashara na uwekezaji, na ufanisi na uadilifu wa serikali. Kwa msisitizo zaidi, orodha ya uhuru wa kiuchumi hupima uhuru wa nguvukazi na masoko ya fedha(Miller na wenzake, 2018). Ili kuchunguza asili yaya uhuru wa kiuchumi, Nikolaev & Bennett (2016) wanapendekeza kwamba pale watu wanapokuwa na maamuzi zaidi juu ya mustakabali wa maisha yao, wanakuwa na kawaida ya kufuatilia ndoto zao vizuri zaidi na kupata mafanikio makubwa zaidi. Kinadharia, uhuru wa kiuchumi huboresha ukuaji na ustawi wa nchi kuruhusu watu kujiamulia mambo yao katika maisha yao. Watu wanaojisimamia wenyewe

wanaweza kufanya kazi mmoja-mmoja au kwa pamoja, kutengeneza bidhaa na kutoa huduma zinazokidhi mahitaji ya soko barabara (Miller na wenzake, 2018). Watu wanaweza kufanya kazi bila kizuizi, kufanya matumizi au kuwekeza katika mkondo wowote wenye manufaa kwao. Matokeo ya jambo hili, huongeza ufanisi wa soko na ukuaji wa kiuchumi (Wu, 2011). Tafiti hizi zinasisitiza kwamba uhuru wa watu kujiamulia mambo yao na kusimamia mustakabali wa maisha yao huboresha viwango vya ubora wa maisha na kwa maana hiyo kuimarisha ukuaji wa kiuchumi. Matokeo ya jambo hili, huwezesha watu kufanya kazi mmoja-mmoja au kwa pamoja na kutengeneza bidhaa na kutoa huduma zinazokidhi mahitaji ya soko (Miller na wenzake, 2018). Pale watu wanapokuwa na uhuru wa kufanya kazi, kufanya matumizi au kuwekeza katika mkondo wowote wenye manufaa kwao, ufanisi wa soko na ukuaji wa kiuchumi vitaongezeka (Wu, 2011).

Manufaa ya kiuchumi yanayoonekana wazi ya uhuru wa kiuchumi yamepelekea uwazi ulioongezeka kwenye biashara na mageuzi mengine yenye mwelekeo wa soko katika nchi zinazoendelea, katika iliyokuwa ngome ya Sovieti ya Ulaya Mashariki, na hata katika nchi zenye uchumi ulioendelea. Kielezi cha ripoti ya uhuru wa kiuchumi kimeiweka Tanzania katika fungu la tatu pamoja na nchi kama vile Kenya, Rwanda, Zambia, Afrika Kusini, Nigeria, na Namibia. Katika ripoti hii, Tanzania ilipata kiwango cha 6.75 na kushika nafasi ya 97 kati ya nchi 165. Katika Afrika kusini mwa Sahara, Tanzania inashika nafasi ya nane kati ya nchi 47 na kiwango chake cha jumla kipo juu ya wastani wa eneo hilo, ingawa kipo chini ya wastani wa dunia. Ripoti imesisitiza kwamba uhuru wa kiuchumi una matokeo makubwa katika kutokomeza umaskini na kuboresha ustawi wa Watanzania. Inakadiriwa kwamba, takribani watu milioni 14 nchini Tanzania wanaishi katika umaskini uliokithiri, na karibia nusu ya watu wanaishi on chini ya 1.90 kwa siku na matarajio ya umri wa kuishi ni miaka 65 (Benki ya Dunia ripoti, 2021).

## 2.0 MALENGO, MITAZAMO NA MBINU

### 2.1 Malengo ya Utafiti

Lengo pana la utafiti huu ni kuchanganua ripoti ya Taasisi ya Fraser iliyotolewa hivi karibuni ya "Orodha ya Nchi kwa Viwango vya Uhuru wa Kiuchumi Duniani", na kufanya uchanganuzi kuchunguza "Kiwango cha Uboreshaji wa Uhuru wa Kiuchumi Tanzania 2021". Kipekee, utafiti huu unafanyia kazi maeneo makuu yafuatayo:

- Kuhakiki na kufanya uchunguzi wa kitaifa juu ya "Uhuru wa kiuchumi nchini Tanzania 2021" kulingana na mapengo yaliyobainika.
- Kuhakiki tafiti nyingine za ndani na kimataifa, kuendesha majadiliano ya mashauriano, mahojiano, na majadiliano ya vikundi lengwa juu ya mada husika kulingana na mapengo yaliyobainika.
- Kupendekeza Mageuzi ya Sera katika maeneo manne, ambayo ni; Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi, Uimara wa Sarafu, Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa na Udhibiti ili yajumuishwe katika Michakato ya Utayarishaji wa Sera nchini Tanzania.
- Kutoa ripoti ya Viwango vya Uhuru wa Kiuchumi nchini Tanzania vilivyo bora zaidi na mapendekezo ya sera kwa ajili ya kuwasilishwa kwa watunga sera.

### 2.2 Mwelekeo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia mwelekeo ufuatao ili kufanikisha utafiti huu: -

- Kufanya tathmini changanuzi ya kina ambayo msingi wake ni ushahidi imara kutoka katika vyanzo vinavyoaminika.
- Mahojiano yanayohusisha mtoa taarifa mkuu taarifa yalifanyika kwa utaratibu maalumu, yakachanganuliwa na kujumuishwa kwenye ripoti.
- Nyenzo zote mbili za changanuzi wa ya kupima ubora na kupima kiasi zilitumika kukuza uchanganuzi wa kimaudhui wa taarifa husika katika zoezi hili.
- Utafiti huu uchanganuzi mpana uliofanyika kwa kina na utokanao na ushahidi.

### 2.3 Mbinu za Utafiti

Mshauri elekezi alitumia mbinu mchanganyiko za utafiti kufanya zoezi hili. Mbinu ya utafiti ya kupima ubora ilitumika kuchukua taarifa kutoka kwenye nyaraka sahihi na watoa taarifa waliochaguliwa. Katika zoezi hili, aina zote mbili za data; data msingi na data sekondari

zilichukuliwa na kuchanganuliwa. Data msingi zilichukuliwa kupitia mahojiano na watoa taarifa wakuu waliochaguliwa kutoka Taasisi za Utafiti, Taasisi za Elimu ya Juu na Sekta binafsi. Vyanzo sekondari kimsingi vilitokana na uhakiki na uchanganuzi wa ripoti ya mwaka 2021 iliyotoa Orodha ya Nchi kwa Viwango vya Uhuru wa Kiuchumi Duniani kutoka na Taasisi ya Fraser. Uchunguzi na uchanganuzi zaidi ulijikita katika vigezo vikuu vifuatavyo vya viwango vya uhuru wa kiuchumi:

- Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi,
- Uimara wa Sarafu,
- Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa, na
- Udhibiti.

Utaratibu uliopelekea kukamilika kwa zoezi unahusisha kufanyika kwa majadiliano na kushirikisha taarifa husika zilizoainishwa kwenye michakato ya utayarishaji wa sera nchini Tanzania na kutoa taarifa ya Viwango vya Uhuru wa Kiuchumi nchini Tanzania vilivyo bora zaidi na mapendekezo ya sera kwa ajili ya kuwasilishwa kwa watunga sera.

# 3.0 UELEWA ULIOPATIKANA KUPITIA VITABU NA MAANDIKO MBALIMBALI

## 3.1 Uhusiano kati ya Uhuru wa Kiuchumi na Ukuaji wa Kiuchumi (pato la taifa)

Tafiti nyingi zimejaribu kufichua asili ya uhusiano kati ya uhuru wa kiuchumi na ukuaji wa kiuchumi. Kwa kutumia aina tofauti za mbinu za mahesabu ya kiuchumi na viashiria tofauti vya uhuru wa kiuchumi, wanazuoni walifanya jaribio la kujibu swali: je, uhuru wa kiuchumi unapelekea ukuaji wa kiuchumi? Tafiti nyingine zimejaribu kubainisha ni sehemu gani ya uhuru wa kiuchumi huchangia ukuaji.

Akin na wenzake (2014) walichunguza matokeo ya uhuru wa kiuchumi kwenye ukuaji wa kiuchumi katika nchi zenye viwango tofauti vya kipato. Walifanya uchanganuzi wa jopo kwa sampuli kielelezo ya nchi 94 kwa kipindi mwaka 2000 hadi 2010. Walihitimisha kwamba katika nchi zote, bila ya kujali kiwango cha kipato, kiwango cha uhuru wa kiuchumi kilikuwa na uhusiano chanya na ukuaji wa kiuchumi, wenye maana kitakwimu.

Richard Cebula (Cebula 2011, 2013; Cebula na Clark 2014; Cebula na Mixon 2012, 2014) walitafiti uhusiano kati ya uhuru wa kiuchumi na hali ya kiuchumi ya Nchi 30 Wanachama wa Umoja wa Mashirikiano ya Kiuchumi na Maendeleo (OECD) na kubaini kwamba uhuru wa kiuchumi ulikuwa na matokeo chanya kwenye kiwango/ukuaji wa pato la taifa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2003 hadi 2007. Kipindi hicho cha mpito was kilichunguzwa kutaka kujua matokeo ya fikra zinazopendelea mabadiliko ya kiuchumi katika utengenezaji wa thamani ya kiuchumi. Pääkkönen (2010) alichunguza jinsi uhuru wa kiuchumi ulivyoonesha kuwa na athari chanya katika ukuaji wa pato la taifa kwa kila mfanyakazi mmoja katika kundi la sampuli kielelezo ya nchi 25 zilizopitia mabadiliko katika kipindi cha kuanzia mwaka 1998 hadi 2005. Bayar (2016) pia alishughulikia matokeo ya uhuru wa kiuchumi kwenye ukuaji wa kiuchumi katika nchi zilizopitia mabadiliko kwa msingi wa data kutoka mwaka 1996 hadi 2012, kwa nchi 11 kama hizo kutoka Umoja wa Ulaya na kuthibitisha nadharia kwamba uhuru wa kiuchumi na biashara ya kimataifa huongeza ukuaji wa kiuchumi.

Gwartney na Lawson (2004) walichunguza matokeo ya uhuru wa kiuchumi kwenye ukuaji wa kiuchumi lakini kwa kuweka mkazo maalumu kwenye uwekezaji na uwezo zalishi. Walibaini kwamba uhuru wa kiuchumi Unachochea uwekezaji kwa nguvu sana. Mataifa yenye kiwango cha uhuru wa kiuchumi chini ya 5 (katika kipimo kinachoanzia sifuri hadi 10, ambapo namba ya juu zaidi inaashiria kiwango cha juu zaidi cha uhuru wa kiuchumi) yalivutia US$845 katika uwekezaji

kwa kila mfanyakazi mmoja kwa kipindi cha kuanzia mwaka 1980 hadi 2000 na US$68 tu kwa kila mfanyakazi mmoja katika uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni. Mataifa yenye kiwango cha uhuru wa kiuchumi juu 7 yalivutia US$10,871 katika uwekezaji kwa kila mfanyakazi mmoja, ikiwa ni pamoja na US$3,117 za uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni.

Halikadhalika, uwekezaji unakuwa na tija zaidi katika mataifa yaliyo huru kiuchumi. Kudumisha vigezo visivyobadilika kunadhaniwa kuwa na matokeo katika ukuaji na uwezo zalishi, kama vile pato la taifa kwa kila mtu, maeneo ya joto, maeneo ya pwani, mabadiliko katika uwekezaji kwa watu, na uwekezaji wa umma, Gwartney na Lawson walibaini kwamba ongezeko la kizio cha asilimia moja katika uwiano baina ya uwekezaji binafsi na pato la taifa hupelekea ongezeko katika kiwango cha ukuaji wa pato la taifa kwa kila mtu kwa kizio cha asilimia 0.33 katika nchi iliyo huru kiuchumi. Ongezeko kama hilo la uwekezaji binafsi katika nchi yenye uhuru wa chini kiuchumi huongeza kiwango cha ukuaji wa pato la taifa kwa kila mtu kwa kizio cha asilimia 0.19. Kwa maneno mengine, uwekezaji katika mataifa yaliyo huru kiuchumi (kwa kiwango kinachozidi 7) ulikuwa na matokeo chanya kwenye ukuaji uliofikia 70% zaidi kuliko uwekezaji katika mataifa yenye viwango hafifu vya uhuru wa kiuchumi (kiwango chini ya 5).

Kwa kurejelea mfano sawa na huo, Gwartney na Lawson walikokotoa pia matokeo ya uhuru wa kiuchumi kwenye ukuaji wa jumla kupitia aina zote mbili za athari za moja kwa moja na zisizokuwa za moja kwa moja. Walibaini kwamba, endapo taifa liliongeza uhuru wake wa kiuchumi kwa kizio kimoja (katika kipimo kinachoanzia sifuri hadi 10) katika miaka ya 1980, lilikuwa na uwezekano wa kuona ongezeko la ukuaji wa kizio cha asilimia 1.9 kwa mwaka kwa kipindi cha kuanzia mwaka 1980 hadi 2000. Kwa sababu ya viwango vya juu vya ukuaji kutokana na uhuru wa kiuchumi, pia walibaini kwamba kwa muda mrefu uhuru wa kiuchumi ni ushahidi wa zaidi ya theluthi mbili ya vigezo vya mabadiliko katika pato la taifa.

Ongezeko katika uhuru wa kiuchumi hupunguza pia umaskini (Norton na Gwartney, 2008).


Kipekee, kiwango umaskini uliopindukia wa $1 kwa siku kilikuwa 29.7% mwaka 2004 katika nchi zenye viwango vya uhuru wa kiuchumi duniani chini ya 5 lakini 7.7% tu katika nchi zenye viwango vya uhuru wa kiuchumi duniani kati ya 6 na 7; kiwango cha umaskini wa $2 kwa siku hushuka kutoka 51.5% hadi 46.2% to 38.9% mtu anapotoka mataifa yenye uhuru finyu na kuhamia mataifa yenye uhuru mkubwa. Halikadhalika, ongezeko la kizio kimojakatika kiwango cha uhuru wa kiuchumi duniani kati ya 1980 na 1995 lilitokana na asilimia kushuka kwa kizio

cha 5.21 katika kiwango cha umaskini wa $1-kwa siku na asilimia kushuka kwa kizio cha 5.22 katika kiwango cha umaskini wa $2 kwa siku.

Norton na Gwartney walichunguza pia uhusiano kati ya uhuru wa kiuchumi na hatua nyingine za ustawi. Katika mataifa yenye uhuru hafifu, 72.6% ya watu walikuwa na uwezekano wa kupata maji salama ikilinganishwa na karibia 100% katika mataifa yenye uhuru wa juu kabisa. Matarajio ya umri wa watu kuishi katika kundi la nchi huru zaidi yalikuwa miaka 20 zaidi kuliko ilivyokuwa kwa wale wanaotoka katika mataifa yenye uhuru duni kabisa. Mataifa mengi yenye uhuru mkubwa zaidi zaidiyalikuwa na mara mbili ya idadi ya madaktari kwa watu 1,000 kuliko mataifa yenye uhuru duni kabisa. Kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa, watoto wadogo 64 zaidi walinusurika na kifo za uzazi katika mataifa mengi yenye uhuru mkubwa zaidi kwa mwaka kuliko ilivyokuwa katika nchi zisizokuwa huru. Kwa kila watoto elfu moja chini ya umri wa miaka mtano, watoto 109 zaidi walinusurika na kifo cha utotoni katika nchi zenye uhuru mkubwa zaidi kila mwaka kuliko katika zile nchi ambazo kwa kiasi kikubwa hazina huru.

Kielelezo 1 kinaonesha pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja (Bei za mwaka 2015 kwa kizio cha US $) kati ya Tanzania, Afrika kusini mwa Sahara, Singapore na Korea Kusini, na nchi nyingine za Dunia (ripoti ya Taasisi ya Frasier, 2022). Kuna uhusiano chanya baina ya ukuaji wa kiuchumi kipimo kwa kutumia pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja na uhuru wa kiuchumi, kwa mfano, Singapore yenye pato la taifa linalofikia dola za Kimarekani bilioni 340 inashika nafasi ya pili, wakati ambapo Hong Kong SAR, China zenye pato la taifa linalofikia dola za Kimarekani bilioni 346.6 zimeendelea kubakia katika nafasi ya kwanza katika orodha ya uhuru wa kiuchumi kwa miaka mitano iliyopita.

Kielelezo 1: Pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja. Bei za mwaka 2015 kwa kizio chaUS$





Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Uhuru wa kiuchumi unachochea ukuaji wa kiuchumi. Kielelezo 1 kinaonesha jinsi uhuru wa kiuchumi ulivyochochea ukuaji na ustawi katika nchi za Singapore na Korea Kusini. Mwaka 1960, Korea Kusini, kufuatia mateso ya kukaliwa kimabavu na vita vya wenyewe kwa wenyewe, ilikuwa maskini zaidi kuliko taifa la wastani kutoka Afrika kusini mwa Sahara. Pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja nchini Korea Kusini (bei za mwaka 2015 kwa kizio cha US$) lilikuwa $1,027 ikilinganishwa na $1,136 taifa la wastani kutoka kusini mwa Sahara. Korea Kusini ilifungua uchumi wake na kutanua uhuru wa kiuchumi. Hadi kufikia mwaka 2020, wastani wa pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja nchini Korea Kusini ulikuwa 2 mara 20 kupita ule wa barani Afrika.

Kielelezo 3b kimejikita kwenye ukuaji wa kiuchumi katika nchi za Afrika kusini mwa Sahara. Kinaonyesha kwamba mwenendo duniani wa uhuru wa kiuchumi kuinua ukuaji unaonekana kuwa kweli barani Afrika. Mataifa yenye viwango vya juu vya uhuru wa kiuchumi, kama Botswana na Cape Verde, yamevuka kwa haraka wastani wa kiwango cha ustawi cha bara la Afrika japokuwa zilianzia chini ya wastani wa kiwango cha ustawi cha kusini mwa Sahara. Kielelezo 2 kinaonyesha kwamba Tanzania, kwa kiasi fulani ikiwa na kiwango cha juu zaidi cha uhuru wa kiuchumi kuliko nchi za kusini mwa Sahara, imeziba kidogo pengo baina yake na nchi nyingine za Afrika lakini bado inajikokota nyuma sana.


Kielelezo 2: Pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja. Bei za mwaka 2015 kwa kizio cha US$




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Uhuru wa kiuchumi unachochea ukuaji wa kiuchumi. Kielelezo 1 kinaonesha jinsi uhuru wa kiuchumi ulivyochochea ukuaji na ustawi katika nchi za Singapore na Korea Kusini. Mwaka 1960, Korea Kusini, kufuatia mateso ya kukaliwa kimabavu na vita vya wenyewe kwa wenyewe, ilikuwa maskini zaidi kuliko taifa la wastani kutoka Afrika kusini mwa Sahara. Pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja nchini Korea Kusini (bei za mwaka 2015 kwa kizio cha US$) lilikuwa $1,027 ikilinganishwa na $1,136 taifa la wastani kutoka kusini mwa Sahara. Korea Kusini ilifungua uchumi wake na kutanua uhuru wa kiuchumi. Hadi kufikia mwaka 2020, wastani wa pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja nchini Korea Kusini ulikuwa 2 mara 20 kupita ule wa barani Afrika.

Kielelezo 3: Pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja. Bei za mwaka 2015 kwa kizio cha US$




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kielelezo 2 kimejikita kwenye ukuaji wa kiuchumi katika nchi za Afrika kusini mwa Sahara. Kinaonyesha kwamba mwenendo duniani wa uhuru wa kiuchumi kuinua ukuaji unaonekana kuwa kweli barani Afrika. Mataifa yenye viwango vya juu vya uhuru wa kiuchumi, kama Botswana na Cape Verde, yamevuka kwa haraka wastani wa kiwango cha ustawi cha bara la Afrika japokuwa zilianzia chini ya wastani wa kiwango cha ustawi cha kusini mwa Sahara. Kielelezo 2 kinaonyesha kwamba Tanzania, kwa kiasi fulani ikiwa na kiwango cha juu zaidi cha uhuru wa kiuchumi kuliko nchi za kusini mwa Sahara, imeziba kidogo pengo baina yake na nchi nyingine za Afrika lakini bado inajikokota nyuma sana.

Matokeo kama hayo yaliripotiwa katika taarifa ya Haydaroglu (2016) kwa nchi za Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini (BRICS). Baasikue, Karabegovic na wenzake (2003) na Bennett (2016) waligundua kwamba kiwango na ukuaji wa uhuru wa kiuchumi vilikuwa na matokeo chanya katika kiwango na ukuaji wa pato la taifa katika mikoa 10 ya Kanada na majimbo 50 ya Marekani kwa kipindi cha kuanzia mwaka 1994 hadi 1999 (na 1981 hadi 1997). Hata hivyo, matokeo ya utafiti kuhusu uhusiano chanya baina ya uhuru na ukuaji wa kiuchumi yanaonesha mapungufu fulani. De Haan na wenzake (2006) walikataa kiwango cha juu cha matokeo ya uhuru wa kiuchumi kwenye ukuaji. Hoja hii is inaungwa mkono na mwenendo wa hivi karibuni na takwimu zilizorekodiwa kwa mfano na Malaysia yenye pato la taifa linalofikia dola za Kimarekani bilioni 336.7 lakini inashika nafasi ya 53 katika kielezo cha uhuru wa kiuchumi duniani (Taasisi ya Fraser, 2020 ripoti).

## 3.2 Ustawi na Uhuru wa Kiuchumi


Shughuli ya kiuchumi kadri inavyoratibiwa kwa “ uchaguzi wa mtu binafsi, biashara inayofanyika kwa hiyari, masoko yaliyo wazi, na haki ya kumiliki ardhi zinazotoa ulinzi wa wazi na kufuatwa”, au kwa maneno mengine, uhuru wa kiuchumi (Gwartney 2009: 939). Tafiti mbalimbali zimeibua hoja kwamba masoko huru na ushindani huchechemua kipato kwa mtu mmoja mmoja au ukuaji wa kiuchumi na zimebaini uhusiano chanya (Murphy 2016; Bennett na wenzake 2017; Murphy na O’Reilly 2018; Spruk na Keševljević 2018).

Kwa kiasi kikubwa, mgawanyo wa kipato unaonekana kutoathiriwa na uhuru wa kiuchumi na masoko yaliyo wazi, kama ambavyo utafiti mwingi wa kiuchumi umeonesha (Sala-i-Martin, 2002). Kwa kweli, katika mataifa yenye uhuru yaliyo huru kabisa kiuchumi, 10% ya watu maskini zaidi hupata mgao wa juu kidogo zaidi wa pato la taifa, 2.92%, kuliko wanavyofanya katika mataifa yenye uhuru finyu, 2.69%, kama inavyoonekana katika Kielelezo 4. Kwa msisitizo zaidi,

kwa sababu ya ustawi ambao uhuru wa kiuchumi huleta kupitia mgao wa pato la taifa na kusababisha matokeo tofauti ya haraka kwa watu maskini katika mataifa yenye uhuru dhidi ya wale wanaotoka katika mataifa yenye uhuru finyu.

Katika mataifa yenye uhuru finyu, 10% ya watu maskini zaidi wana wastani wa kipato cha $1,736 tu kwa mwaka (ingawa hii kwa mara nyingine inatia chumvi wastani wa kipato, kama Korea Kaskazini na Cuba, zisizojumuishwa katika orodha kutokana na ukosefu wa data). Katika mataifa yenye uhuru mkubwa sana, 10% ya watu maskini zaidi wana wastani wa kipato cha $14,204, zaidi ya mara nane ya kipato cha mataifa yenye uhuru finyu.


Kielelezo 4: Mgawanyo wa Kipato kwa Robo




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kielelezo kinaonyesha kwamba uhuru wa kiuchumi hupunguza umaskini kwa kasi. Katika mataifa yenye uhuru finyu, zaidi ya asilimia 30 ya watu wanakabiliwa na umaskini uliokithiri (uliotafsiriwa kama US$1.90 kwa siku) na nusu ya watu wanakabiliwa na umaskini wa kadiri (US$3.20 kwa siku). Katika mataifa yenye uhuru mkubwa sana, asilimia mbili tu ya watu ndio wanaokabiliwa na umaskini wa $1.90 na chini ya asilimia tano ndio wanaokabiliwa na umaskini wa $3.20.

Kielelezo 5: Mgawanyo wa Kipato kwa Quartile (Bei za mwaka 2017 kwa kizio cha PPP$)





Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Tafiti nyingine zimeibua hoja kwamba uhuru wa kiuchumi huchechemua hali ya kuridhika na maisha na zimeonesha kwamba kuna uhusiano chanya baina ya mambo hayo (Veenhoven 2000; Ovaska na Takashima 2006; Gropper na wenzake 2011; Gehring 2013; Graafand na Compen 2015) kama ilivyo katika (vipimo kadhaa vya) ustawi wa kihisia(Nikolaev na Bennett 2017).

Wapinzania wa uhuru wa kiuchumi wameibua hoja kwamba ustawi unaoletwa na uhuru wa kiuchumi siyo kipimo kizuri cha ustawi wa watu; kwamba badala yake, hatuna budi kushughulika na furaha ya watu na wanadai kwamba, inapatikana kwa kiwango cha juu zaidi katika mataifa ya kijamaa. Ni kawaida kwa hoja hii kutolewa bila ya ushahidi wowote. Kinyume chake, idadi ya kutosha ya tafiti inaonyesha sasa kwamba uhuru wa kiuchumi "husababisha" furaha (au hali ya kuridhika na maisha). Kielelezo 6 kinaonesha furaha ilivyopimwa kwenye Kielezo cha Furaha cha Umoja wa Mataifa kwa kipimo cha 0 hadi 10, ambapo 10 inaashiria kiwango kiwango cha juu zaidi cha furaha. Kama ilivyojitokeza, watu wanapenda kuwa na uwezo wa kujipangia mambo yao wenyewe.

Kielelezo 6: Kielezo cha Furaha




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Hall na Lawson (2014) ulibaini, hata hivyo, kwamba uhuru zaidi wa kiuchumi unaendana na taarifa mbaya binafsi ya hali ya afya (wakati huohuo kupunguza tofauti za kiafya kati ya wazungu na watu weusi). Halikadhalika, pia walibaini kwamba taarifa binafsi za afya zilizoripotiwa zina uhusiano chanya na kipato, jambo linaloweza kuashiria kwamba uhuru wa kiuchumi una matokeo chanya yasiyo ya moja kwa moja kwenye afya. Tafiti nyingine zimeibua hoja kwamba uhuru wa kiuchumi unaweza pia kuchochea elimu; Feldman (2017) alibaini uhusiano chanya baina ya uhuru wa kiuchumi na uwekezaji katika mtaji-watu.


Mahusiano chanya kati ya uhuru wa kiuchumi na elimu yalibainishwa pia na King na wenzake (2012). Kupitia elimu, uhuru wa kiuchumi unaweza pia kuinua ushiriki wa umma. Hartmann na Uhlenbruck (2015) walibaini uhusiano chanya kati ya uhuru wa kiuchumi na uwajibikaji wa makampuni wa kurudisha sehemu ya faida katika utunzaji wa mazingira. The sababu inaweza kuwa kwamba uhuru wa kiuchumi huchechemua utatuzi wa kijasiriamali wa matatizo kama vile ongezeko la joto duniani na ulinzi wa mazingira. Ulinzi wa haki ya kumiliki ardhi huchochea makampuni uwekezaji wa siku za baadaye katika nishati zisizoharibu mazingira, kwa kuwa kuna uhakika zaidi kwamba yatapata manufaa kutoka katika mapato ya hivi vitega uchumi. Wakati utafiti wa kichunguzi uliofanywa na Nikolaev (2014) ukiashiria uhusiano chanya baina ya uhuru wa kiuchumi na ustawi kama ilivyopimwa na Kielezo cha Maisha Bora cha OECD, matokeo ya utafiti wake yanaonesha kubaini jambo moja la kipekee, ambalo ni usawa baina ya maisha ya kazi na maisha binafsi.

Block na wenzake (2018) pia walibaini kwamba wajasiriamali wanapitia usawa duni baina ya maisha ya kazi na maisha binafsi, kwa sababu kitendo cha mtu kuwa bosi wake yeye mwenyewe hupelekea mtu huyo kufanya kazi kwa nguvu zaidi kuliko mwajiriwa wa mshahara (McCloskey 2006). zaidiZaidi ya hayo, kutokana na ushindani, makampuni makubwa hupendelea zaidi waajiriwa wanaofanya kazi kwa saa nyingi kwa ajili ya kupata ujira mwingi kadri inavyowezekana kutoka kwao (Schor 1993). Matokeo yake, watu wanaweza kujikuta wanafanya kazi saa nyingi sana kwakwa wiki wakiweka rehani mambo mengine muhimu sana katika maisha yao, kama vile mahusiano ya familia, kwa ajili ya tunzo ya kifedha ambayo, endapo wakiifikiria sana, wanaweza kutambua kwamba hawaihitaji. Biashara huria (mojamoja kati ya vipimo vyauhuru wa kiuchumi) inaweza pia kuvuruga usawa baina ya maisha ya kazi na maisha binafsi.

Katika mataifa yenye uhuru wa kweli wa kiuchumi, watu wanatendewa kwa usawa kama watu, siyo kama tabaka la upendeleo unaoangalia kabila, dini, rangi au jinsia. Kielezi cha Umoja wa

Mataifa cha Kutokuwa na Usawa wa Kijinsia hupima hali ya kutokuwa sawa kwa kipimo cha 0 (usawa kamili wa kijinsia) hadi 1 (hali iliyokithiri ya kutokuwa sawa) kama inavyoonekana katika Kielelezo 7. Mataifa yenye uhuru duni kiuchumi yana kiwango cha 0.51, kiwango cha juu kupita kiasi cha hali ya kutokuwa sawa kijinsia, wakati ambapo mataifa yenye uhuru mkubwa sana yana kiwango cha 0.17.

Kielelezo 7: Kielezi cha Umoja wa Mataifa cha Kutokuwa na Usawa wa Kijinsia





Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

## 4.0 MATOKEO YA UTAFITI

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya utafiti kutoka katika uchanganuzi uliotokana na msingi wa malengo makuu ya utafiti huu kwa kuzingatia maeneo matano yauhuru wa kiuchumi. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita kwenye maeneo manne, ambayo ni; Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi, Uimara wa Sarafu, Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa na Udhibiti. Matokeo ya utafiti katika kielelezo1 chini yanatoa taarifa kwa mapana jinsi Tanzania inavyofanya katika kila eneo la uhuru wa kiuchumi, na kwa maana hiyo mwanzo wa tathmini ya utendaji kwa watengenezaji wa sera juu ya maeneo yanayohitaji kuboreshwa na aina ya maboresho yanayohitajika. Kwa bahati mbaya, uhuru wa kiuchumi nchini Tanzania, licha ya maboresho, umebaki katika viwango vya chini duniani, nafasi ya 99 katika orodha ya nchi 165. Tazama Kielelezo 8. Kielezi kinaiweka Tanzania kwenye nafasi ya chini sana katika sbaadhi ya maeneo ikiwemo uhuru wa kufanya biashara, nafasi ya 112, na udhibiti wa biashara, nafasi ya 127.


Kielelezo 8: Nafasi ya Tanzania katika Uhuru wa Kiuchumi




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kielelezo 9 kinalinganisha kiwango cha Tanzania katika uhuru wa kiuchumi na nchi nyingine pamoja na wastani wa maeneo mengine ya kikanda. Kiwango cha Tanzania kinaendelea kubaki chini ya wastani wa dunia na chini zaidi ya mataifa yenye viwango vya juu vya uhuru wa kiuchumi, kama vile Korea Kusini na Singapore.


Kielelezo 9: Uhuru wa Kiuchumi kwa Nyakati




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kielelezo 10 kimejikita kwenye Afrika. Tanzania imeendelea kubaki nyuma sana ya Botswana, nchi inayofanya vizuri sana kwa miaka kwenye uhuru wa kiuchumi katika nchi za Afrika kusini mwa Sahara. Tanzania imepitwa pia na Cape Verde.

Kielelezo 10: Mkazo wa Uhuru wa Kiuchumi Afrika




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

## 4.2 Tanzania 2021 "Kielezi cha Uhuru wa Kiuchumi" katika Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi

Sura hii imebeba maelezo uchunguzi na uchanganuzi wa kina wa vielezi vikuu vya uhuru wa kiuchumi kwa msingi wana ripoti ya Taasisi ya Fraser ikifanya marejeo makuu kwenye kielezi cha uhuru wa kiuchumi Tanzania 2021 kuhusiana na Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi na vielezi vyake vidogo. Katika eneo muhimu sana la mfumo wa kisheria na haki ya kumiliki ardhi; kielezi kinaiweka Tanzania kwenye nafasi ya 72. Eneo hili halina budi kuboreshwa endapo Tanzania inataka kutengeneza fursa na mustakabali wenye fanaka kwa wananchi wake. Utawala thabiti unaozingatia sheria na unaotoa haki sawa kwa wote ni kigezo kimoja chenye umuhimu mkubwa wa lazima katika kuchochea maendeleo. Utafiti umeonesha kwamba kuboresha utawala unaozingatia sheria ni moja kati ya changamoto kubwa kuliko zote ambazo serikali yoyote inaweza kukumbana nayo.

Matokeo ya utafiti katika Jedwali 1 umeonesha tofauti kubwa ya mabadiliko katika idadi kuhusiana na kuaminika kwa polisi.

Mwaka 2015, tarakimu ya kiwango ilikuwa 5.45, ikipanda hadi 5.63 mwaka 2016 na 5.65 mwaka 2017 na kushuka hadi 5.16 mwaka 2018 na 2019. Mabadiliko haya yanaweza kuelezewa kwa mwenendo fulani katika mageuzi kadhaa yaliyokuwa yanatokea ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ambapo Jeshi la Polisi linawajibika kwa changamoto za kidunia zinazoendana na waasi katika Nchi za jirani, kwa mfano katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Msumbiji. Nchini, kulikuwa na kiasi fulani cha kutotengemaa visiwani Zanzibar kilichopelekea tume ya uchaguzi visiwani Zanzibar kubatilisha matokeo uchaguzi, na ambapo Chama cha Wananchi

(CUF) kiligomea uchaguzi wa marudio . Kushuka kwa kiwango mwaka 2019 kunaweza kuwa kulichochewa na matukio ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019.

Jedwali 1: Muundo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi nchini Tanzania

| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumo wa Kisheria & Haki ya Kumiliki Ardhi | 5.53 | 5.56 | 5.57 | 5.31 | 5.3 | 5.39 |
| Uhuru wa mahakama | 5.72 | 5.68 | 5.55 | 5.29 | 5.4 | 5.64 |
| Haki jinai na Mahakama zisizopendelea | 4.59 | 4.73 | 4.8 | 4.68 | 4.67 | 4.46 |
| Ulinzi wa haki ya kumiliki ardhi | 4.93 | 5.06 | 5.09 | 4.83 | 4.83 | 4.83 |
| Jeshi kuingilia utawala unaozingatia sheria na siasa | 6.67 | 6.67 | 6.67 | 5.8 | 5.83 | 5.83 |
| Uadilifu wa mfumo wa kisheria | 6.67 | 6.8 | 6.83 | 6.64 | 6.42 | 7.14 |
| Utekelezaji wa mikataba kisheria | 5.71 | 5.71 | 5.71 | 5.71 | 5.71 | 5.71 |
| Vikwazo vya udhibiti kwenye mauzo ya mali | 7.29 | 7.02 | 7.02 | 7.02 | 7.02 | 7.02 |
| Kuaminika kwa polisi | 5.45 | 5.63 | 5.65 | 5.16 | 5.16 | 5.16 |
| Marekebisho ya sheria za haki kijinsia | 0.88 | 0.88 | 0.88 | 0.88 | 0.88 | 0.88 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kwa upande wa jeshi kuingilia utawala unaozingatia sheria na siasa katika miaka iliyopita ya hivi karibuni, Tanzania haijapitia a mazingira ya jeshi kuingilia utawala unaozingatia sheria na siasa. Tarakimu haikubadilika mwaka 2015, 2016 na 2017 ikiwa 6.67.


Kama inavyoonesha katika Jedwali 1, Ufanisi wa Tanzania kuhusiana na mfumo wa kisheria na haki ya kumiliki ardhi uliendelea, kwa kiasi fulani, kubakia katika kiwango kilekile huku kiwango cha juu zaidi kikiwa ni 5.57 mwaka 2017 na kiwango cha chini zaidi kikiwa ni 5.3 mwaka 2019, kiwango cha mabadiliko kilikuwa 0.27. Kiwango cha uhuru wa mahakama kilikuwa 5.29 na 5.4 mwaka 2018 na 2019 mtawalia. Uendeshaji usio na tija wa mashtaka kwa makosa ya jinai, uliotokana na kutokuwa huru au kukosa uwezo, hauwezi kuchunguza na kuendesha kesi za rushwa kwa ufanisi, kwa maana hiyo unadhoofisha ufanisi wa jumla wa jitihada za Serikali kupambana na rushwa. Halikadhalika, mfumo wa mahakama unaofanya kazi bila ya kuzingatia viwango hauwezi kujenga na kudumisha imani ya umma katika sifa ya haki na kutokuwa na

upendeleo wa maamuzi na matokeo yake. Mfumo wa aina hiyo umeendelea pia kutokuwa salama dhidi ya ushawishi usiostahili au uliovuka mipaka kutoka nje ya muundo wa kitaasisi au kutoka kwa watu binafsi.

### 4.2.1 Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi

Uadilifu, uhuru na kutoa haki bila upendeleo ni masharti makuu ya lazima ya kuasisi wenye tija na idara tendaji ya mahakama na mfumo mzima wa mahakama kwa utatuzi wa mizozo ya kisheria kwa njia ya amani. Kuasisiwa kwa mfumo unaojitegemea na wenye tija wa kutoa haki unaolinda haki za binadamu huwezesha haki kupatikana kwa wote na kuwa kimbilio bila kificho wala upendeleo ndio tunu inayotafutwa duniani kote.

Kielelezo 11 Mfumo wa kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kwa mujibu wa ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) kama inavyoonekana katika Kielelezo 11, kulikuwa na kushuka kwa ujumla kwa Tanzania katika mfumo wa kisheria na haki ya kumiliki ardhi. Ufanisi uliongezeka mwaka 2015 kutoka 5.53 hadi 5.57 mwaka 2017. Kulikuwa na kushuka katika utekelezaji wa mfumo wa kisheria na haki ya kumiliki ardhi kutoka 5.57 kulikorekodiwa mwaka 2017 hadi 5.3 kama ilivyodhihirika mwaka 2019. Kushuka huko kwa sehemu fulani kulitokana na marekebisho namba 1 ya sheria mbalimbali ya 2018 seksheni za 45 na 120 za Sheria ya Ardhi, 1999 na kutunga seksheni mpya za 120A, 120B, 120C, 120D na 120E. Vikwazo vilivyoanzishwa vilielekeza matumizi ya fedha zilizokopwa na wamiliki wa ardhi. Kabla ya marekebisho haya, wamiliki wa ardhi waliruhusiwa kutumia fedha za mkopo uliopatikana

kutoka taasisi za fedha kuweka rehani ardhi zao. Marekebisho haya yanaanzisha baadhi ya vikwazo katika muktadha huo.

Kwanza, yanatoa haki kwa wamiliki wa ardhi kuweka rehani ardhi zao kwa madhumuni ya kupata mikopo kutoka mabenki au taasisi za fedha, zikiwemo za ndani na hata za kimataifa. Pili, kuna vikwazo kwenye matumizi ya mikopo iliyotolewa; marekebisho yanatamka kwamba wamiliki wa ardhi wanaweza tu kutumia mikopo yao kupitia ardhi iliyowekwa rehani (i) pale ambapo tayari ardhi imeendelezwa, kwa maendeleo zaidi au madhumuni ya uwekezaji mwingine wowote, (ii) pale ambapo ardhi haijaendelezwa au imeendelezwa kidogo, mikopo itumike kwa maendeleo ya sehemu au eneo lote la ardhi hiyo iliyowekwa rehani. Sharti hili lina maana kwamba mikopo, kwa kutumia ardhi kama dhamana, ni sharti itolewe kwa madhumuni ya kuendeleza ardhi iliyowekwa rehani tu. Mtu anaweza kusema kwamba kikwazo hiki ni njia nyingine ya kulinda mabenki na taasisi za fedha na kuhakikisha kwamba fedha zilizokopwa haziwezi kuwekezwa katika biashara nyingine, jambo linaloweza kufanya ulipaji kuwa mgumu kwa mabenki ambayo baadaye hujikuta na na dhamana ambazo thamani yake haiwezi kufidia madeni ya waweka rehani. Kwa kuongezea, masharti haya yamelenga kuwapa wawekewa rehani nafasi ya kuongeza thamani ya mali zao ziliyowekwa rehani kwa matakwa kwamba, mara baada ya kupokea fedha kutoka benki, mweka rehani anatakiwa kwa mujibu wa sheria kutoa taarifa kwa Kamishna wa Ardhi jinsi fedha ilivyowekezwa katika kuendeleza ardhi iliyowekwa rehani.


Sheria chini ya seksheni mpya ya 120B inaweka ukomo wa eneo la kijiografia la mahali ambapo fedha iliyopatikana kwa njia ya rehani inapoweza kutumika, kwa kutamka kwamba inapaswa tu kuwekezwa nchini Tanzania na inawataka wawekewa rehani kuwasilisha kwa Kamishna wa Ardhi tamko la kuthibitisha kwamba fedha iliyotolewa, kwa hakika, imewekezwa katika ardhi ile. Wenye haki ya matumizi ya ardhi na wawekezaji wanalazimika kutekeleza marekebisho haya, kwa kuwa kushindwa kutimiza matakwa yake itapelekea uvunjaji wa masharti ya haki ya matumizi ya ardhi, jambo ambalo hatimaye linaweza kupelekea kubatilishwa kwake. Marekebisho ya sheria yanaendelea kutamka kwambakwamba utaratibu mzima na utekelezaji wa masharti kuhusiana na ardhi kuwekwa rehani chini ya seksheni 120A na 120B vitaongozwa na kanuzi zitakazotolewa baadaye. Marekebisho yalikuja na lengo la kupunguza the hatari za kifedha kwa mabenki kutokana na mikopo isiyolipwa kwa kuhakikisha kwamba mikopo inayochukuliwa inaelekezwa kwa hakika kwenye miradi iliyokusudiwa. Ingawa sheria ina dhamira njema kwa mabenki, bado haijasaidia kutatuamasuala yanayohusiana na mikopo

isiyolipwa kwa sababu masuala haya yanaathiriwa na vigezo ikiwemo mbalimbali, lakini siyo ukomo wake, masuala ya kiuchumi, soko na utekelezaji sahihi wa mikakati.

#### 4.2.2 Uhuru wa Mahakama

Uhuru wa idara ya mahakama nchini Tanzania umewekwa na katiba na kwa mujibu wa sheria. Ieleweke kwamba, uhuru wa idara ya mahakama ni uhuru wa mahakama katika mchakato wa utoaji wa haki, na mahakama zinalazimika kutekeleza tu masharti ya katiba na sheria za ardhi. Uhuru huu wa idara ya mahakama uliohakikishwa nakatiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatuacha na changamoto kubwa ya endapo ni ukweli au kitu cha kufikirika kutokana na asili ya mambo yanayoendelea katika mfumo wa mahakama kuhusiana uhuru wake katika utaratibu wa kutoahaki.

Kielelezo 12 Uhuru wa mahakama




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Matokeo katika Kielelezo 12 yanaonesha mwelekeo katika uhuru wa mahakama, uchanganuzi ukithibitisha kwamba, kulikuwa na kiasi kikubwa cha kushuka kwa uhuru katika mfumo wa mahakama kutoka 5.72 kama ilivyodhihirika mwaka 2015 hadi 5.29 ilivyoorekodiwa mwaka 2018. Hali hii inaweza kufafanuliwa kwa vigezo kadhaa vinavyodhoofisha uhuru wa idara ya mahakama kulingana na wanazuoni mbalimbali, akiwemo "Chris Maina" walioviweka katika makundi mawili; vigezo vya ndani na vigezo vya nje. Hata hivyo, kinyume na vigezo vilivyotajwa hapo awali, tarakimu ya kiwango ilipanda hadi 5.4 mwaka 2019. Matokeo ya utafiti yanakinzana na yale yaliyonakiliwa Kenya katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Masharikikati ya kipindi

kilekile ambapo ufanisi wake ulikuwa 2 015 (5.37), 2016 (5.48), 2017 (5.59), 2018 (5.24) na 2019 (5.24). Tarakimu hizi zinaonesha tofauti ndogo katika ufanisi kwa sababu nyingi miongoni mwa nchi katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zina mwenendo unaofanana wa kijamii na kiuchumi kama vile matumizi ya rushwa, na ujira duni wa Maofisa wa mahakama (Hakimu) unaoambatana na gharama za juu za maisha.

Vigezo vya ndani ni yale masuala yanayodhoofisha uhuru wa idara ya mahakama ikiwemo: -watumishi wa mahakama wasio na uwezo kukingiwa kifua na maofisa fulani wa vyeo vya juu katika idara ya mahakama au serikalini (Vigogo); maofisa wa mahakama kutopewa kipaumbele kupitia ujira duni au usiotosheleza na kuwaacha katika hali ngumu wa kiuchumi; na tafsiri finyu ya nadharia ya uhuru wa mahakama. Kwa kiasi kikubwa, hii ni inatokana na sharti la katiba kuwa la ujumla sana kiasi cha kutoa mwanya wa tafsiri nyingi. Hali hii hupelekea pia mazingira rushwa.

Vigezo vya nje vinavyodhoofisha uhuru wa idara ya mahakama vinajumuisha - mwenendo wa ujumla ambapo Serikali kama mihimili wa Dola ulitwaa madaraka makubwa na kuipuuza mihimili mingine katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2020. Mamlaka ya juu kabisa ya Dola (Serikali) yalitwaa madaraka juu ya Idara ya mahakama kiasi kwamba kupitia uteuzi wa jaji mkuu na majaji wa mahakama kuu kufanywa na Rais; uteuzi wa wakaguzi wa mahakama katika mahakama za mwanzo na mahakama kuu na mazoea ya Serikali to kuzishawishi mahakama kutoa hukumu zinazoipendelea bila ya kuzingatia sheria na kanuni za haki ya asili. Kwa kuongezea, chini ya vigezo vya nje; kuna suala la usumbufu kwa watumishi wa mahakama ambao kwa kiasi kikubwa hufanywa na Serikali kama wa Dola katika kesi mbalimbali. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2020 kulikuwa na kasi ya kushuka kwa hali ya kuheshimu katiba au sheria kama ilivyoonekana kwa kuwafukuza kazi watumishi wa ngazi za juu serikalini katika mikutano ya hadhara kinyume na kanuni za utumishi wa umma na orodha ndefu ya makosa yasiyo na dhamana chini ya Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu iliyotumiwa katika kesi dhidi ya wapinzani wa kisiasa wa Serikali, akiwemo Erick Kabendera na Tito Magoti (Shivji, 2021).


#### 4.2.3 Uadilifu wa Mfumo wa Kisheria

Neno uadilifu linatafsiriwa kama dhana nzima inayomaanisha uwezo wa mfumo wa mahakama au mtumishi mmoja-mmoja wa idara ya mahakama kukataa rushwa, wakati huohuo akiheshimu kikamilifu tunu za uhuru, kutoa haki bila upendeleo, uadilifu wa mtu binafsi, kufuata utaratibu kwa usahihi, usawa, weledi na bidii ya kazi. Kitendo cha rushwa katika hatua moja ya mnyororo

wa haki jinai kinaweza kusababisha madhara makubwa katika mchakato mzima au hata kubatilisha dhima yake na kupoteza imani ya umma katika sheria na taratibu zake. Changamoto katika kudai haki na utekelezaji wa mikataba katika mashauri ya mahakama vinaweza kupelekea mazingira ya kutokuwa na uhakika na mwenendo wa kisheria na hatimaye kutishia biashara, kuvunja moyo wa kijasiriamali na uwekezaji. Kupuuza matumizi sawa ya sheria hudhoofisha uhalali wa taasisi za umma na kuchangia watu kufanya makosa bila woga.

Matokeo ya utafiti katika Kielelezo 13 cha ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) kuhusiana na uadilifu wa mfumo wa kisheria yaliashiria kiasi kikubwa cha kushuka kwa kiwango cha 0.41 kutoka 2017 hadi 2019 kuhusiana na uadilifu wa mfumo wa kisheria nchini Tanzania.

Kielelezo 13 Uadilifu wa Mfumo wa Kisheria




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021)

Matokeo ya utafiti hapo juu yalitokana na vigezo kadhaa kama vile rushwa, ambapo rushwa imeendelea kuwa tatizo la kimfumo, na jitihada za mageuzi zimezaa matokeo mchanganyiko. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeshutumiwa kwa kutilia mkazo rushwa ndogondogo na kutojishughulisha sana na vitendo vya rushwa vya maofisa wa ngazi za juu.

Tanzania ilikuwa nafasi ya 87 katika orodha ya nchi 180 kwenye ripoti ya Viwango vya Rushwa katika Sekta ya Umma iliyotolewa na Transparency International. Kwa mujibu wa Transparency international, Tanzania imepunguza kiwango cha rushwa katika miaka ya ya hivi karibuni lakini

rushwa imeendelea kuwa kikwazo kikubwa cha ukuaji. Matokeo ya uhuru wa kiuchumi kwenye rushwa yanahitaji kusisitizwa. Kuongezeka kwa uhuru wa kiuchumi hupunguza rushwa. Ukosefu wakwa uhuru wa kiuchumi ndiyo malighafi ya rushwa. Endapo unahitaji kuomba ruhusa ya mtu fulani ili ufanye jambo fulani, tayari kuna mtu fulani wa kuomba rushwa.


Mwaka 2020, kashfa kadhaa ziliibuka ambapo wahusika waliobainika walikabiliwa na hatua za kisheria, lakini hata hivyo zilitoa taswira mbaya ya uwezo wa mamlaka za serikali kutumia kikamilifu nguvu walizopewa. Mwezi Julai, maofisa tisa wa ngazi za juu wa TAKUKURU walimamishwa kazi kwa tuhuma za rushwa kuhusiana na ujenzi wa majengo ya taasisi hiyo. Mwezi Desemba 22 maofisa wa ngazi za juu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) walimamishwa kazi, kupisha uchunguzi wa rushwa kubwa. Ripoti ya ukaguzi wa fedha ya mwaka 2018 ilionesha upotevu wa mapato yanayofikia $ milioni 640 kwa mwaka wa fedha 2016–17. Ukaguzi zaidi mwaka 2019 ulifichua zaidi ya $ bilioni 1 kupotea au kutumika vibaya. Wito wa Upande wa upinzani wa kuchapisha ripoti kamili ya mkaguzi mkuu na kutoa msukumo wa uwajibikaji ulikataliwa. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali alikana upotevu wowote au wizi.

Matokeo haya yanaonesha kwamba Idara ya Mahakama Tanzania inakabiliwa na uhaba wa fedha pamoja na rushwa. Majaji ni wateule wa kisiasa, na Idara ya mahakama haina bajeti inayojitegemea, jambo linaloifanya kutokuwa salama dhidi ya shinikizo la kisiasa. Matokeo ya shinikizo hilo yanaonekana wazi katika kesi zinazowahusu wanasiasa kutoka upande wa upinzani na wakosoaji wengine wa Serikali, pamoja na upepo wa hivi karibuni mabadiliko ya sheria ili kukandamiza ushindani huru na wa haki na kulinda watawala dhidi ya kushtakiwa.

#### 4.2.4 Ulinzi wa Haki ya Kumiliki Ardhi

Haki ya Ardhi inasimamiwa na Ibara ya 24 ya katiba inayoweka takwa la haki ya kumiliki ardhi kisheria na kutoa ulinzi ardhi hiyo. Katiba ya Tanzania, 1977 inatamka kwamba, “kila mtu nchini Tanzania amepewa haki ya kumiliki ardhi”. Haki ya mtu kumiliki ardhi inasimamiwa na na sharti ya Sheria ya Ardhi na Vijiji.1999. Sheria hizi zote mbili zilibatilisha desturi za kimila na kibaguzi zilizokuwa na matokeo hasi katika haki ya wanawake kumiliki ardhi. Sheria hizi zinatambua haki sawa kwa wanaume na wanawake kumiliki ardhi.

Kielelezo 14: Ulinzi wa haki ya kumiliki ardhi




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kama inavyooneshwa katika matokeo ya utafiti kwenye Kielelezo 14, ulinzi wa haki ya kumiliki ardhi ulionesha wigo wa mabadiliko kati ya 2015 ambapo kiwango kilikuwa 4.93 hadi kufikia ongezeko la 0.79 mwaka 2017, kiwango kilishuka zaidi hadi 4.83 mwaka 2018 na 2019. Kuna baadhi ya matukio ambapo Serikali imetumia masharti yenye utata ya sheria na kanuni kupokonya rasilimali na ardhi ya wanasiasa wenye uwezo wa kifedha kutoka upande wa upinzani, aikiwa ni pamoja na mali za Freeman Mbowe zilizopo Hai na Dar es Salaam. Japokuwa Watanzania wana haki ya kuanzisha biashara binafsi, mara nyingi wanatakiwa kulipa rushwa katika mchakato wa kupata leseni na kufanya shughuli za kibiashara.

Serikali inamiliki ardhi yote na huikodisha kwa watu na makampuni binafsi, kitu kinachopelekea vurugu juu ya haki ya ardhi kati ya wananchi na makampuni ya uchimbaji wa madini. Ulinzi wa mali za Mashirika na Asasi za Kiraia ulishuka kwani baadhi ya mashirika hayo yalikuta akaunti zao za benki zikiwa zimefungwa wakati ambapo mengine yaligeuka wahanga wa kila aina ya madai kutoka mamlaka za mapato. Hata mali za wafanya biashara zilizuiliwa kwa kile kilichodaiwa ni ukwepaji wa kodi na kusababisha hatari katika haki ya kumiliki ardhi.

### 4.2.5 Marekebisho ya sheria za haki kijinsia

Katika kielezi cha Kutokuwa na Usawa wa Kijinsia, kinachopima kuona kama wanawake wana uhuru sawa wa kiuchumi baina yao na wanaume, Tanzania inashika nafasi ya 91. Hii inamaanisha kwamba nusu ya watu inakabiliwa na vikwazo katika kujaribu kujenga mustakabali bora zaidi

kwa ajili yao wenyewe na Taifa. Marekebisho ya hali ya Kutokuwa na Usawa wa Kijinsia hatua mpya ya kupima kiasi cha uhuru wa kiuchumi kwa wanawake, kuona kama sheria za nchi zinawatendea wanawake kwa usawa katika mambo ya kiuchumi; kwa mfano, kuanzisha biashara, ajira, na kadhalika. Kinapimwa kuanzia sifuri hadi moja. Wakati kiwango cha Tanzania cha 0.88 kinaweza kuonekana kuwa vizuri, nchi inashika nafasi ya 91 duniani kwa kuwa mataifa mengine yamechukua hatua za haraka zaidi kufuta sheria zinazozuia uhuru wa kiuchumi kwa wanawake. Ni muhimu kufuta sheria zinazopunguza uhuru wa wanawake. Kuweka ukomo kwenye uhuru wa kiuchumi kwa wanawake ni kama kujaribu kuendesha pikipiki kwa gurudumu moja. Inazui a vikali nguvu na ukuaji wa kiuchumi.

Uchanganuzi unaendelea kuashiria kwamba, Tanzania inafanya vizuri kuliko Kenya na Uganda ambazo viwango vyake vilikwamia 0.76 kwa kipindi hichohicho, ingawa nchi kama Marekani, Uingereza, na Denmark ilifanya vizuri zaidi kwa kupata 1.0 kwa kipindi hichohicho. Hii kwa sehemu fulani ni kwa sababu idadi kubwa kiasi ya wanawake hawana uwezo wa kufanikisha haki yao kumiliki ardhi na mali nyingine kutokana na ukosefu wa uelewa wa sheria hizi na jinsi ya kuzitekeleza. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakataza aina zote za ubaguzi, na Haki za wanawake zimethibitishwa kikatiba lakini hazilindwi kwa ulinganifu. Wanawake wanakabiliwa na ubaguzi wa kimfumo katika ajira, ikiwemo unyanyasaji wa kingono, jambo ambalo ni nadra kuongelewa kupitia mikondo rasmi kisheria.


Kama ilivyobainishwa katika tafiti kadhaa, ifuatayo ni baadhi ya mifano ya masuala ya ardhi/mali nchini Tanzania. Wanawake wengi nchini Tanzania wana uwezo wa kupata ardhi kupitia waume zao au ndugu zao wa kiume. Hata hivyo, hawamiliki wao mwenyewe; mabinti ambao hawajaolewa, wajane na wanawake waliochana na waume zao mara nyingi ni wahanga unyanyapaa, ubaguzi na unyanyasaji unaofanywa na ndugu zao wa kiume; na waume hutumia hati za ardhi kujipatia mikopo bila ya kuwahusisha, wake zao, jambo linalosababisha kuondolewa katika makazi na/au kupoteza mali zao. Katika mambo ya urithi, kumekuwa na mgawanyo usio sawa wa mali kati ya wanaume na wanawake ambapo wanawake daima huchukuliwa kama watu wa daraja la pili. Kwa kuwa ndoa za kimila hazisajiliwi, wanawake hupata hasara inapotokea talaka au vifo vya waume zao na hujikuta wakipoteza karibia kila kitu.

Hali ngumu ya kijamii na kiuchumi kwa wanawake inajitokeza zaidi katika maeneo ya vijijini na katika uchumi usio rasmi.

### 4.2.6 Haki Jinai na Mahakama Zisizopendelea

Mfumo wa haki jinai unaweza kuwa madhubuti lakini bila ya kutoa haki kama inavyoweza kutokea chini ya mazingira ya utawala usio wa kidemokrasia; mfumo usio wa haki wa kiuchumi uliotokana na hali iliyokithiri ya kutokuwa sawa na kukosekana kwa usawa; siasa kuingia katika maamuzi ya mahakama; kuenea kwa rushwa mahakamani; sheria na taratibu zilizopitwa na wakati; mafunzo duni kwa majaji; mahakama kutojitosheleza kwa rasilimali; na polisi wasiotenda haki na maamuzi na mazoea ya uendeshaji wa mashtaka. Ujira duni pia unashawishi rushwa na kuwavunja moyo wanasheria wengi weledi na waadilifu kuomba ajira katika idara ya mahakama. Mapungufu haya yanapaswa kushughulikiwa kwa ajili ya kukuza uhuru wa mahakama. Mahakama za chini zinaendelea kutumia sheria za mila, lakini mara nyingi hukomea katika masuala ya madai.

Kielelezo 15: Haki Jinai na Mahakama Jisizopendelea




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Uadilifu wa mahakama daima huendana na idara ya mahakama ya nchi, na chimbuko lake ni hali ya kukosa ufanisi na ukosefu wa polisi na taratibu zinazofaa za uendeshaji wa mashtaka. Matokeo ya utafiti huu utafiti katika Kielelezo 15 yanaonesha kwamba kulikuwa na maendeleo ya ujumla katikakiwango kati ya mwaka 2015 na 2017 wakati ambapo ufanisi uliongezeka kwa tofauti ya 0.21. Hata hivyo kiwango kilishuka kwa 0.26 kati ya 2017 na 2018. Mabadiliko haya yanaweza kufafanuliwa kwa hali ya kutokuwa na uhakika katika maamuzi ya kesi; katika matukio mengi, ucheleweshaji wa kesi na mrundikano wa kesi mara nyingi vilikuwa ni matokeo ya polisi na taratibu za uendeshaji wa mashtaka, uzembe na kutofanya kazi kwa ufanisi, mambo yanayoambatana na upungufu wa rasilimali watu, ukosefu wa weledi na vitendea kazi katika Idara ya mahakama.


Suala linalopuuzwa kuliko yote katika muundo wa kitaasisi na sera kuhusiana na na Idara ya Mahakama nchini Tanzania ni lile la usimamizi na uwajibikaji. Kuna hitaji la kuwa na utaratibu wa haki na wenye tija ndani ya Idara ya Mahakama utakaotumika kwa ajili ya kusimamia mwenendo na ufanisi wa majaji na kuchukua zinazofaa hatua kama vile motisha na hatua za kinidhamu. Katika utafiti huu, tunahitimisha kwa kutilia mkazo kwenye ukweli kwamba uhuru wa mahakama ndiyo njia pekee ya kupata matokeo bora, yakijulikana kama uadilifu wa mahakama na utoaji wa haki bila upendeleo, ambayo ni mambo ya muhimu na lazima.

### 4.2.7 Utekelezaji wa Mikataba Kisheria

Mkataba unatekelezeka endapo mahakama ipo radhi kutaka pande zote mbili kutekeleza masharti ya makubaliano. Utekelezaji wa mikataba na utatuzi wa mizozo ni mambo ya kutazamwa sana kwa ajili ya utendaji sahihi wa soko. Ili kuanzisha mkataba, ni sharti kuwe na ofa kutoka upande mmoja ikifuatiwa na ridhaa ya upande mwingine. Utekelezaji wa mkataba muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi. Biashara ndiyo kitu kinachowezesha makampuni makubwa na watu binafsi kujipambanua, na kubobea katika eneo fulani la utaalanu, au mgawanyo wa nguvukazi kama Adam Smith alivyoongelea katika kitabu cha Utajiri wa Mataifa, 1776, ni msingi wa uwezo zalishi na kwa maana hiyo ukuaji wa kiuchumi.

Mahakama ndiyo taasisi muhimu kuliko zote ya umma ya utekelezaji wa mikataba. Siyo tu kwa sababu ndiyo kimbilio la mwisho katika tukio la ukiukwaji wa mikataba bali pia kwa sababu tishio la kushtakiwa linaweza kupunguza ukiukwaji. Kama inavyooneshwa katika Kielelezo 16, hapajakuwa na mabadiliko uingiaji wa mikataba ya kisheria; kiwango hakikubadilika (5.71) katika kipindi cha miaka 5 kutoka 2015 hadi 2019.

Kielelezo 16: Utekelezaji wa Mikataba Kisheria



Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021)

Taratibu za mahakama hazina budi kurahisishwa na usimamizi na mchakato wa kesi kuwa katika mfumo unaojiendesha. Ingawa mageuzi mahakama yapo chini ya Idara ya Mahakama, Serikali inaweza kuonesha mfano kwa kuhakikisha kwamba matumizi yake ya mahakama yanafaa na kuendana na maslahi mapana zaidi ya umma. Siyo mizozo yote yote inahitaji kupelekwa mahakamani kwa utatuzi. Kuna fursa za usuluhishi, upatanishi, maelewano nje ya mahakama, na mibadala miingine ya mahakama.

### 4.2.8 Ulinganishi wa Nchi katika Utawala Unaozingatia Sheria na Haki ya Kumiliki Ardhi

Tanzania inafanya vibaya sana katika utawala unaozingatia sheria, nafasi ya 72 duniani. Ipo nyuma sana katika sampuli zote za kielelezo cha mataifa, wastani wa dunia, ingawa kwa kiasi fulani ikiwa imevuka ya wastani wa Afrika Mashariki na kusini mwa Sahara, tazama Jedwali 2. Uchumi wenye tija wa soko hauwezekani bila ya mfumo wa kisheria imara na wenye kutabirika unaolinda haki ya kumiliki ardhi na utekelezaji wa mikataba kwa wote, kwa usawa na kwa haki. Maboresho katika eneo hili ni changamoto kubwa kuliko zote na fursa kwa Tanzania. Hakuna taifa, isipokuwa labda baadhi ya mataifa yenye utajiri wa mafuta, lililofikia hali ya tajiri bila ya utawala imara unaozingatia sheria.

Jedwali 2: Ulinganishi wa Nchi katika Utawala Unaozingatia Sheria na Haki ya Kumiliki Ardhi

| Na | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Uswisi | 8.59 | 8.54 | 9.04 | 10.00 | 8.83 | 6.25 | 9.60 | 9.05 | 1.00 | 8.74 |
| 2 | New Zealand | 8.66 | 8.48 | 8.09 | 10.00 | 8.77 | 7.18 | 9.90 | 8.68 | 1.00 | 8.72 |
| 3 | Finland | 8.57 | 8.67 | 9.34 | 10.00 | 9.64 | 6.29 | 7.52 | 9.54 | 1.00 | 8.70 |
| 4 | Denmark | 8.55 | 8.36 | 8.33 | 10.00 | 9.62 | 6.57 | 9.73 | 8.09 | 1.00 | 8.66 |
| 5 | Iceland | 7.93 | 8.36 | 8.20 | 10.00 | 9.05 | 6.78 | 8.75 | 9.02 | 1.00 | 8.51 |
| 6 | Uholanzi | 8.04 | 8.23 | 8.48 | 10.00 | 9.25 | 6.57 | 7.95 | 8.32 | 1.00 | 8.35 |
| 7 | Australia | 8.44 | 7.57 | 8.45 | 10.00 | 8.92 | 6.76 | 8.14 | 8.42 | 1.00 | 8.34 |
| 8 | Singapore | 6.40 | 8.47 | 8.94 | 8.33 | 8.21 | 7.83 | 8.96 | 9.19 | 1.00 | 8.29 |
| 9 | Kanada | 7.67 | 7.84 | 7.72 | 10.00 | 8.51 | 5.82 | 8.68 | 7.92 | 1.00 | 8.02 |
| 10 | Estonia | 7.79 | 7.17 | 7.38 | 8.33 | 7.73 | 5.98 | 9.50 | 8.31 | 1.00 | 7.78 |
| 11 | 10 za juu | 8.06 | 8.17 | 8.40 | 9.67 | 8.85 | 6.60 | 8.87 | 8.65 | 1.00 | 8.41 |
| 12 | Wastani wa | 5.54 | 4.99 | 5.51 | 6.38 | 5.90 | 4.36 | 7.59 | 5.62 | 0.87 | 5.36 |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Dunia | | | | | | | | | | |
| 13 | Botswana | 6.80 | 6.36 | 6.52 | 8.33 | 6.68 | 3.07 | 7.81 | 6.30 | 0.88 | 6.10 |
| 14 | Cape Verde | 6.55 | 5.80 | 5.44 | | 7.43 | 6.06 | 8.92 | 5.55 | 1.00 | 6.54 |
| 15 | Korea Kusini. | 6.06 | 6.74 | 6.69 | 6.67 | 8.04 | 6.88 | 8.22 | 7.24 | 0.88 | 6.65 |
| 16 | Afrika Mashariki | 4.59 | 4.15 | 4.70 | 4.38 | 4.79 | 3.93 | 7.76 | 5.09 | 0.86 | 4.66 |
| 17 | Kusini mwa Sahara | 4.98 | 4.11 | 4.54 | 4.60 | 5.14 | 3.54 | 6.78 | 4.89 | 0.79 | 4.37 |
| 18 | Tanzania | 5.64 | 4.46 | 4.83 | 5.83 | 7.14 | 5.71 | 7.02 | 5.16 | 0.88 | 5.39 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Tanzania ina viwango vibaya sana karibia katika maeneo yote makuu ya utawala unaozingatia sheria: Uhuru wa mahakama, mahakama zisizopendelea, na ulinzi wa mali binafsi, jeshi kujiingiza, na uadilifu katika mfumo wa kisheria, utekelezaji wa mikataba, na kuaminika kwa polisi. Watu, hasa maskini na wasio na uwezo, hawana uhakika wa kulindwa kwa haki na uhuru wao kwa mujibu wa sheria endapo mfumo wa kisheria unakosa uhuru, hali ya kutoa haki bila upendeleo, na uadilifu na mali binafsi siyo hazilindwi.

Uwezekano wa jeshi kujiingiza unaweza pia kudhoofisha mfumo wa kisheria.

Utekelezaji wa mkataba ni muhimu sana, utekelezaji dhaifu wa mikataba unawavunja moyo watu na wafanya biashara kuingia kwenye mikataba iliyokubaliwa kwa uhuru, kwa kuwa unaziacha pande husika bila uhakika wa endapo mikataba itafuatwa kwa haki na mizozo kushughulikiwa kwa usahihi na mfumo wa kisheria. Hali hiyo ya kutokuwa na uhakika hupunguza nafasi ya makubaliano yaliyofikiwa kwa uhuru. Ukosefu wa kuaminika kwa polisi na gharama kubwa ya kushughulika na uhalifu huongeza mzigo wa gharama kwa mfanyabiashara, huongeza hatari, na mbaya zaidi huwaacha watu wanaofanya biashara katika mazingira ya vurugu na uharibifu. Yote haya hutoa mianya ya rushwa na upendeleo kwa matajiri na wenye madaraka kwa kuwa ulinzi wa kisheria ni dhaifu. Ingawa Tanzania imeboresha kidogo katika miaka ya hivi karibuni, mfumo wa kisheria ulikumbwa na mdororo mkubwa sana kwenye miaka ya 2000. Jaribio tu la kurudi kwenye mstari litakuwa ni hatua nzuri ya kusonga mbele lakini hatua zaidi zinahitajika kwa ajili ya Tanzania kukua na kufikia ustawi kamili.

### 4.3 Uwezo wa Kuwa na Uimara wa Sarafu

Katika sUimara wa Sarafu, Tanzania inashika nafasi ya 91, Taifa limeshuhudia mfumuko mkubwa wa bei na kutotengemaa kwa fedha katika miaka iliyopita na lilikuwa bado katika mfumuko wa bei wa digiti mbili hadi hivi karibuni katika miaka ya 2010. Tanzania imeboresha ufanisi wake katika miaka ya hivi karibuni lakini mfumuko wa bei umeendelea kuwa mkubwa kupita kiasi, unaosababisha tishio la mfumuko wa juu zaidi wa bei wakati ambapo dunia inakabiliwa na tatizo kubwa la mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei au kutotengemaa katika ugavi wa fedha vinaweza kudhoofisha manufaa yatokanayo na biashara. Katika kiashiria hiki, vielezi vikuu vifuatavyo vitabainishwa; ukuaji wa fedha; kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka kwa mfumuko wa bei; mfumuko wa bei (mwaka wa hivi karibuni zaidi); na uhuru wa kumiliki akaunti za benki katika fedha za kigeni. Hata hivyo, matokeo ya utafiti katika Jedwali 3 yanaonesha kwamba, uimara wa sarafu uliendelea, kwa kiasi fulani, kubakia katika kiwango kilekile huku kiwango cha juu zaidi kikiwa 8.24 mwaka 2018 na kiwango cha chini zaidi kikiwa ni 8.06 mwaka 2015.

Jedwali 3: Uwezo wa Kuwa na Uimara wa Sarafu


| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Uimara wa Sarafu | 8.06 | 8.22 | 8.23 | 8.24 | 8.20 | 8.34 |
| Ukuaji wa fedha | 9.39 | 9.92 | 9.79 | 9.33 | 9.16 | 10 |
| Kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka kwa mfumuko wa bei | 8.97 | 9.00 | 9.21 | 9.34 | 9.34 | 9.03 |
| Mfumuko wa bei | 8.88 | 8.97 | 8.94 | 9.30 | 9.31 | 9.34 |
| Uhuru wa kumiliki akaunti za benki katika fedha za kigeni | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

### 4.3.1 Ukuaji wa fedha

Ukuaji wa fedha ni ongezeko katika kiasi cha fedha katika uchumi: Ukisukumwa na kiasi kikubwa cha biashara ya nje, ukuaji wa fedha umekuwa mkubwa katika miaka miwili iliyopita. Ongezeko katika ugavi wa fedha hufanya kazi katika njia zote mbili za kushusha viwango vya riba, jambo linalochochea uwekezaji, na kuweka fedha zaidi katika wanunuzi, kuwafanya wajione kuwa tajiri zaidi, na kwa maana hiyo kuchochea matumizi. Kama ilivyodhihirika katika ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) katika Kielelezo 17, kulikuwa na mabadiliko katika ukuaji wa fedha kati ya 2015 (9.39), 9.92 mwaka 2016 hadi 9.16 mwaka 2019, mabadiliko haya yanaweza kufafanuliwa kwa kwa sehemu fulani kutokana na mabadiliko kwenye kanuni ya fedha inayoshughulika na miamala na uhamishaji wa pesa taslimu.

Kielelezo 17: Ukuaji wa fedha




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Katika mifano mingi, makampuni makubwa ya biashara huitikia ongezeko la mauzo kwa kuagiza malighafi zaidi na kuongeza uzalishaji. Ongezeko katika ugavi wa fedha kwa kawaida hushusha viwango vya riba, matokeo yake, hupelekea uwekezaji zaidi na fedha zaidi katika wanunuzi, hivyo kuchochea matumizi. Wafanya biashara huitikia kwa kuagiza malighafi zaidi na kuongeza uzalishaji. Ongezeko la shughuli za biashara huongeza hitaji la nguvukazi. Kinyume chake kinaweza kutokea endapo ugavi wa fedha unapoanguka au pale kiwango cha ukuaji wake kinaposhuka. Kushuka katika ukuaji wa fedha kama ilivyooneshwa katika kielelezo 5 kulitokana na mtikisiko wa jumla wa uchumi wa dunia uliopelekea ugavi wa fedha iliyosababishwa na matokeo ya Uviko-19. Fedha hizo ziliambatana na vikwazo kwenye biashara ya kimataifa.

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia (2021), Ukusanyaji wa viashiria vya maendeleo ulichukua kutoka vyanzo vinavyotambulika rasmi, ukuaji wa fedha (% kwa mwaka) nchini Tanzania uliripotiwa kuwa 5.6773% mwaka 2020. Mikopo ya ndani iliyotolewa kwa sekta binafsi na Serikali Kuu kutoka mfumo wa mabenki ulikua kwa 14.9% katikamwaka ulioishia Desemba 2021, ikilinganishwa na 10.8% mwaka uliotangulia. Mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi ilirejea katika viwango vya kabla ya janga, ikirekodiwa ukuaji wa 10% kwa mwaka mwezi Desemba 2021 ikilinganishwa na 7.8% katika uliotangulia na 3.1% mwezi Desemba 2020. Kutengemaa upya kwa mikopo ya sekta binafsi kwa kiasi kikubwa ilitokana na kudumishwa kwa sera jumuishi ya fedha na kuboresha mazingira ya kufanya biashara yaliyoathiriwa vibaya ya janga la UVIKO-19. Mikopo mingi kwa sekta binafsi kilielekezwa katika biashara, shughuli binafsi hasa shughuli za viwango vya chini na kati, uzalishaji wa viwandani na shughuli za uchimbaji wa madini. Shughuli binafsi za watu, biashara, uzalishaji wa viwandani na kilimo vlilendelea kuwa wanufaika wakuu katika muktadha wa mgao wa mikopo iliyotolewa na mabenki kwa sekta binafsi.

Kwa mujibu wa Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (2020/2021) uliotolewa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, kiwango cha ufanisi wa uchumi kilikuwa cha kutosha ndani ya kigezo kilichokusudiwa kwa mwaka 2019/20, kufuatia utekelezaji wa sera jumuishi ya fedha. Kwa maana hiyo, ukuaji wa hatua zote za ugavi wa fedha uilendelea kuwa mpana kadri ya malengo ya 2019/20. Kwa wastani, ugavi mpana zaidi wa fedha (M3) ulikua kwa asilimia 9.9 katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.0, na ulipanda juu zaidi ya asilimia 4.9 ilivyoorekodiwa katika kama hicho cha kipindi mwaka 2018/19. Ukuaji mkubwa zaidi wa fedha (M2) ulikuwa kwa asilimia 11.4 ikilinganishwa na asilimia 5.2 mwaka 2018/19, wakati ambapo wastani wa hifadhi ya fedha ulikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 0.4.

Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa imara kwa wastani wa asilimia 8.7 ikilinganishwa na asilimia 6.5. Kiasi kikubwa cha mgao wa mikopo kwa sekta binafsi kilielekezwa katika shughuli binafsi za kiuchumi, biashara, uzalishaji wa viwandani na kilimo. Mwaka 2020/21, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unakadiriwa kuendelea kuwa mkubwa, takribani kwa asilimia 11.6. Makadirio yanajumuisha sera jumuishi ya fedha na hatua za sera za benki kuu ya fedha zinazotekelezwa ili kuilinda sekta ya kifedha na uchumi kufuatia matokeo ya UVIKO-19, na kurejesha hali ya kawaida ya shughuli zilizokuwa zimeathiriwa na janga hili, kama vile kuanza tena kwa utalii, michezo na burudani na elimu.

Shughuli zinazogusa bajeti ya Serikali kwa msingi wa pesa taslimu ziliendelea katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Aprili 2020, licha ya kukabiliana na changamoto fulani zilizosababishwa na mlipuko wa UVIKO-19 juu ya minyororo ya ugavi na uhitaji. Mapato ya ndani ya Serikali yanayofikia TZS bilioni 16,238.0, ambayo yalikuwa ni asilimia 95.5 ya makadirio, na asilimi 10.5 juu zaidi ya mapato kama hayo katika kipindi kama hicho cha mwaka 2018/19. Ufanisi mzuri ulitokana na usimamizi wa kodi ulioimarishwa. Matumizi kwa msingi wa pesa taslimu yanayofikia TZS bilioni 18,281.1, ambayo kati yake TZS bilioni 5,284.9 zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika kushughulikia changamoto za kiuchumi kutokana na janga la UVIKO, serikali, pamoja na mambo mengine, iliongeza matumizi katika sekta ya afya na ulinzi wa mahitaji ya kijamii, iliondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na ushuru wa forodha kwenye vifaa tiba, na kuweka kipaumbele katika ulipaji wa madeni kwa sekta ya biashara (Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki Kuu ya Tanzania, 2021)


Deni la serikali, la nje na la ndani, lilibaki katika kiwango himilivu, dola za Kimarekanicha dola za Kimarekani milioni 24,179.5 mwishoni mwa Aprili 2020, kutoka dola za Kimarekani milioni 23,215.4 mwishoni mwa Juni 2019. Deni la nje lilifikia asilimia 73.2 ya deni la serikali. Nakisi ya malipo ya nje ya malipo ilionesha ziada ya dola za Kimarekani milioni 897.1 katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Aprili 2020 ikilinganishwa na upungufu wa dola za Kimarekani milioni 1,082.3 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2018/19, ikisababishwa na kupunguza pengo la upungufu katika miamala ya taifa dhidi ya mataifa mengine duniani.

Maboresho katika salio la miamala ya taifa dhidi ya mataifa mengine duniani kwa kiasi kikubwa lilifafanuliwa kwa ongezeko katika biashara ya nje, hasa dhahabu na korosho. Akiba ya fedha za kigeni ilieindelea kuwa ya kutosha, ikifikia kiasi cha dola za Kimarekani 5,334.3 milioni mwishoni mwa Aprili 2020 kutoka dola za Kimarekani 4,432.6 milioni mwezi Juni 2019. Hifadhi hiyo ilikuwa inatosheleza kukidhi takribani miezi 6.1 ya kiwango kinachokadiriwa cha biashara ya kutoka nje ya bidhaa na huduma, dhidi ya kiwango cha msingi cha walau miezi 4.0. Mwaka 2020/21, mapato ya biashara ya nje kutokana na utalii yanakadiriwa kushuka, kwa kiasi kikubwa kutokana na matokeo yaliyosababishwa na UVIKO-19. Bei za mafuta katika soko la dunia zinakadiriwa kuendelea kuwa chini, wakati ambapo bei za dhahabu zinakadiriwa kuendelea kuwa juu

### 4.3.2 Mfumuko wa Bei

Nchini Tanzania, Kipimo Kikuu cha Mfumuko wa Bei Kitaifa (NCPI) hupima mabadiliko kwa kipindi cha muda fulani katika gharama isiyobadilika ya bidhaa na huduma zinazonunuliwa kwa sampuli wakilishi ya kielelezo cha kaya. Matokeo ya kielezi hupatikana kwa msingi wa matumizi ya kaya kutoka maeneo yote mawili ya mjini na vijijini katika maeneo 25 ya kijiografia. Matokeo ya utafiti kutoka katika ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) kama inavyoonekana katika Kielelezo 18 kuhusuana na mfumuko wa bei (katika mwaka wa hivi karibuni zaidi), matokeo ya utafiti yanaonesha kiwango cha mabadiliko kwa kiasi fulani kwenye mfumuko wa bei kama inavyoonekana katika mfululizo huu kuanzia mwaka mwaka 2015 (8.88), 2016 (8.97), 2017 (8.94), 2018 (9.3) na 2019 (9.31). Inaweza kutafsiriwa kwamba, kiwango cha mfumuko wa bei kilikaribia kudhibitiwa kati ya 2015 na 2017. Kiwango cha mfumuko wa bei kikubwa kiasi mwaka 2018 kutokana na bei za juu za vyakula zilizotokana na uzalishaji wa chini wa mazao ya chakula, wakati ambapo kilikuwa pia kikubwa mwaka 2019 kwa sehemu fulani kutokana na athari za janga la Uviko-19 duniani lenye athari kwenye biashara duniani.

Kielelezo 18: Viwango vya Mfumuko wa Bei




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kwa mujibu wa ripoti ya Ofisi ya Takwimu Tanzania (2021), mfumuko wa bei kwa mwaka kwa mwezi Juni 2022 ulikuwa asilimia 4.4. Mfumuko wa bei ulikuwa mdogo na kudhibitiwa kipindi chote cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikichochewa na upatikanaji wa kutosha wa chakula katika sehemu nyingi za nchi, sera wekevu ya fedha ya benki kuu na sera ya serikali ya fedha, bei za chini za mafuta na nishati ya kutosha. Kielezo cha bei ya mtumiaji (CPI) kwa miezi kumi na mbili kinaonesha jumla ya mfumuko wa bei katika uchumi ilikuwa katika wastani wa asilimia 3.6

katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikilinganishwa na asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2018/19. Kiwango cha chini zaidi cha mfumuko wa bei kilikuwa asilimia 3.3 mwezi Aprili 2020, wakati ambapo kiwango cha juu zaidi kilikuwa asilimia 3.8 mwezi Novemba na Desemba 2019. Mfumuko wa bei za vyakula ulikuwa katika wastani wa asilimia 5.0 ikilinganishwa na asilimia 1.2 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2018/19. Mfumuko wa bei za bidhaa zisizokuwa za vyakula ulishuka hadi kufikia wastani wa asilimia 2.8 kutoka asilimia 5.1 (Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki Kuu ya Tanzania, 2021).

Mfumuko wa bei usiohusisha chakula na nishati, nao pia ulikuwa mdogo na kudhibitiwa katika wastani wa asilimia 2.4 ikilinganishwa na asilimia 2.7. Jumla ya mfumuko wa bei katika uchumi ilikuwa chini ya lengo la nchi la asilimia 5.0, na ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC kiwango cha msingi kisichozidi asilimia 8.0 na asilimia 3.0 - 7.0 mtawalia. Mfumuko wa bei unakadiriwa kuendelea kuwa chini ya lengo la muda wa kati lengo la asilimia 5.0 mwaka 2020/21, kutokana na upatikanaji wa kutosha wa chakula, msukumo wa taratibu katika uhitaji wa bidhaa na huduma, bei za chini za mafuta katika soko la dunia na nishati ya uhakika. Utekelezaji wekevu wa sera ya fedha ya benki kuu na sera ya serikali ya fedha utaongeza kichocheo cha vigezo vinavyotarajiwa kuchangia katika mfumuko mdogo wa bei (Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki Kuu ya Tanzania, 2021).


Katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Aprili 2020, Kielezo cha Bei ya Mtumiaji (CPI) kilionesha mfumuko wa bei ulikuwa wa taratibu katika nchi zenye uchumi ulioendelea, ikisababishwa nakushuka kwa jumla ya uhitaji, wakati ambapo kwa ujumla ulipanda katika masoko yanayochipukia na nchi zinazoendelea kutokana na ongezeko katika bei za vyakula. Katika nchi zenye uchumi ulioendelea, kielezo cha bei ya mtumiaji (CPI) cha mfumuko wa bei kilikuwa katika wastani wa asilimia 1.2, na katika masoko yanayochipukia na nchi zinazoendelea kilikuwa katika wastani wa asilimia 4.5. Katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) , mfumuko wa bei ulikuwa katika wastani wa asilimia 4.2, ukipanda kutoka asilimia 1.9 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2018/19 kwa kiasi kikubwa ilitokana na bei za juu zaidi za vyakula. Hata hivyo, kiwango kilikuwa chini ya kiwango cha msingi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki cha asilimia 8.0. Katika eneo la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kiwango cha mfumuko wa bei kilikuwa kikubwa, wastani wa asilimia 9.3 39.3 kutoka asilimia 9.8, kwa kiasi kikubwa ikichangiwa na mfumuko mkali wa bei katika sbaadhi ya nchi, tazama Jedwali 17. Shirika la Fedha Ulimwenguni linakadiria mfumuko wa bei katika nchi zenye uchumi

ulioendelea na masoko yanayochipukia na nchi zinazoendelea utafikia wastani wa asilimia 0.5 na asilimia 4.6 mwaka 2020 mtawalia kutokana na kushuka kwa bei za nishati. Katika eneo la Afrika kusini mwa Sahara, mfumuko wa bei ulikadiriwa kupanda hadi asilimia 9.3 mwaka 2020 kutoka asilimia 8.4 mwaka 2019, zaidi kutokana na ongezeko tarajiwa katika gharama za chakula katika sehemu sfulani za bara (Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki Kuu ya Tanzania, 2021).

### 4.3.3 Kiasi kinachokubalika cha Kupanda na Kushuka kwa Mfumuko wa Bei

Kipimo cha vigezo vinavyoathiri ukuaji ni msingi wa matokeo ya utafiti. Kwa kawaida, vigezo vya mfumuko wa bei hupimwa kwa kibadala au kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka kwa mfumuko wa bei. Hata hivyo, kibadala cha mfumuko wa bei kinawiana sana kiwango chake, kufanya iwe vigumu kutofautisha athari kwenye ongezeko la kiwango cha mfumuko wa bei na athari za vigezo vya mfumuko wa bei (Khan na Senhadji, 2016). Ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) katika Kielelezo 19 juu ya kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka kwa mfumuko wa bei inathibitisha kwamba, kati ya 2018 na 2019 kulikuwa na mabadiliko kidogo katika kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka kwa mfumuko wa bei kinachofikia 0.03.

Kielelezo 19: Kiasi kinachokubalika cha Kupanda na kushuka kwa Mfumuko wa bei




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kiwango cha mfumuko wa bei kwa mwaka kiliongezeka hadi 4.4% mwezi Juni 2022, kiwango cha juu zaidi tangu Novemba 2017, kutoka 4% katika uliotangulia. Bei zilipanda kwa kasi hasa zaidi katika usafiri (8.9% dhidi ya 7.2% mwezi Mei); chakula & vinywaji visivyokuwa na ulevi (5.9% dhidi ya 5.5%) na nyumba & huduma za umma (4.6% dhidi ya 4.3%). Kwa msingi wa mwezi hadi

mwezi, bei za mnunuzi zilipanda kwa 0.5%, kasi ileile kama ilivyokuwa katika uliotangulia mwezi.

Mfumuko wa bei uilendelea kuwa mdogo na chini ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0, mwelekeo wa kigezo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki kisichozidi asilimia 8.0 na kiwango cha msingi cha SADC cha kati ya asilimia 3.0 na 7.0. Jumla ya mfumuko wa bei katika uchumi kwa miezi kumi na mbili ilikuwa katika wastani wa asilimia 3.6 katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikilinganishwa na asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2018/19. Mfumuko mdogo wa bei na uliodhibitiwa ulitokana zaidi na upatikanaji wa kutosha wa chakula ndani ya nchi, sera wekevu ya fedha ya benki kuu na sera ya serikali ya fedha, nishati ya ukahika, na kushuka sana kwa bei za mafuta katika soko la dunia. Vivyo hivyo, mfumuko wa bei usiohusisha chakula na nishati ulikuwa mdogo, wastani wa asilimia 2.4 ikilinganishwa na asilimia 2.7. Mfumuko wa bei unakadiriwa kuendelea kuwa takribani lengo la muda wa kati lengo la asilimia 5.0, katika wigo wa 3.0 asilimia hadi asilimia 5.0 mwaka 2020/21, kutokana na upatikanaji wa kutosha wa chakula ndani ya nchi, bei za chini za mafuta katika soko la dunia, uhitaji wa taratibu, nishati ya uhakika na sera wekevu ya fedha ya benki kuu na sera ya serikali ya fedha.


#### 4.3.4 Uhuru wa Kumiliki Akaunti za Benki kwa Fedha za Kigeni

Idara ya Benki na Fedha na Biashara ya Break through Attorneys inatoa mwanga juu ya kanuni ya uendeshaji wa akaunti katika fedha za kigeni kwa wakazi wa Tanzania na hatua za udhibiti wa Benki Kuu ya Tanzania kwenye matumizi ya fedha za kigeni pamoja na miamala ya kimataifa. Kwa ujumla, mabenki na taasisi za fedha nchini Tanzania wameruhusiwa kutoa huduma ya fedha za kigeni kwa wakazi katika miamala yote na uhamishaji wa fedha kutoka na kwenda mataifa mengine duniani. Kifungu 2.1 cha Waraka juu ya Fedha za Kigeni inadhibiti miamala ya kitaifa kutoka na kwenda mataifa mengine duniani inatamka kwamba; “Kama kanuni ya jumla, mabenki na taasisi za fedha wanaruhusiwa kutoa huduma ya fedha za kigeni kwa wakazi kuhusiana na malipo yote ya ya ndani na kigeni na uhamishaji wa fedha bila ukomo wowote wa juu, isipokuwa inapokuwa kwa ajili ya kusafiri nje ya nchi ambapo ukomo wa juu wa dola za Marekani 10,000 kwa mtu binafsi utaendelea kutumika”.

Kwa maana hiyo, mabenki na taasisi za fedha zinazowapa wakazi fedha hizo za kigeni zitatakiwa kuzingatia taratibu wekevu za kawaida za kibenki, na kutimiza masharti yafuatayo ya matakwa ya jumla; utoaji wa ushahidi unaofaa wa kimaandishi unaoambatana na ombi wakati wa kutoa

huduma ya fedha za kigeni kwa mwombaji. Mabenki na taasisi za fedha kubaki na nyaraka zilizotajwa hapo awali kwa nia ya kufanyiwa uhakiki na Benki Kuu ya Tanzania katika utaratibu majukumu yake wekevu ya udhibiti ni sharti la lazima. Uhamishaji wa fedha pia unaruhusiwa chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, 2006. Ibara ya 24 (1) (d) ya Sheria hii inaongelea huduma ya utumaji wa fedha kama mojakati ya huduma zitakazotolewa na benki au taasisi ya fedha yenye leseni. Tathmini ya matokeo ya utafiti kwenye Kielelezo 20 yanaonesha kwamba, uhuru wa kumiliki akaunti ya benki katika fedha za kigeni uliripotiwa kutobadilika (5.00) kutoka 2015 hadi 2019, hii ni kwa sababu hapakuwa na mabadiliko yoyote katika udhibiti wa Serikali unaohusiana na umiliki na uendeshaji wa akaunti za benki katika fedha za kigeni.

Kielelezo 20: Uhuru wa Kumiliki Akaunti ya Benki katika Fedha za Kigeni




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kanuni Mpya za Fedha za Kigeni zilizotolewa na Gavana wawa Benki Kuu ya Tanzania (2022) kwa madaraka yake chini ya ibara ya 6 ya Sheria ya Biashara ya Fedha za Kigeni zilianza kutumika tarehe 13 Mei 2022. Kifungu 3(2) cha Kanuni kinatamka kwamba wakazi wanaosafiri nje ya nchi wanaweza kupata fedha za kigeni kutoka benki, taasisi ya fedha au duka la kubadilisha fedha kwa kiasi kisichozidi dola za Kimarekani 10,000. Ikumbukwe kwamba ukomo sawa na huo unatekelezwa chini ya Sheria ya Biashara ya Fedha za Kigeni (Maduka ya Kubadilisha Fedha), (2015). Mbaya zaidi, pamoja na masharti hapo juu na kabla ya kutolewa kwa kiasi kilichotajwa, mkazi atatakiwa kuwasilisha ushahidi wa kimaandishi wa eneo la makazi na nyaraka halali za kusafiria.

Kanuni zimepiga marufuku wakazi kufungua au kumiliki akaunti ya benki nje ya Tanzania isipokuwa kunapokuwa na uhamishaji wa dhamana katika eneo lililotajwa (nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki au nchi ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika) au mtu anapopata ruhusa ya Gavana. Kanuni inamtambua mkazi kama mtu anayeishi kwa mwendelezo au ambaye kituo chake kikuu cha maslahi ya kiuchumi kipo Jamhuri ya Muungano kwa miezi kumi na mbili au zaidi. Ingawa Kanuni hizi zimeendelea kutumika bila ya kufanyiwa majaribio, ingeweza kutafsiriwa kwamba mtaalamu wa kigeni anayefanya kazi nchini Tanzania kwa zaidi ya miezi kumi na mbili anaweza kuzuiwa kuwa na akaunti ya kigeni katika benki ya nchi aliyotoka bila ya ruhusa ya Gavana.

Sheria inamtaka muuzaji wa bidhaa nje kufanya mauzo ya fedha za kigeni kupitia benki ambayo muuzaji wa bidhaa nje ana akaunti. Mbaya zaidi, benki zimepiga marufuku kununua fedha za kigeni kutoka kwa muuzaji wa bidhaa nje asiye na akaunti katika benki hiyo na kuweka matakwa ya lazima ya malipo yanayofanywa na wasiokuwa wakazi kufanyika kupitia mabenki tu. ZaidiHalikadhalika, kanuni ya 11 inaweka kikwazo katika usawazishaji madai ya fedha. Inatamka kwamba pale ambapo b muamala wa iashara ya nje unafanyika kati ya makampuni tanzu, muuzaji wa bidhaa nje anatakiwa kuhakikisha kwamba hakuna usawazishaji madai ya fedha. Ingawa kanuni inamhitaji mwagizaji wa bidhaa kufanya malipo ya biashara ya bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kupitia benki, kanuni 13(2) inamruhusu mwagizaji wa bidhaa kutoka nje kutumia njia nyingine za malipo pale ambapo thamani ya bidhaa kutoka nje haizidi dola za Kimarekani 10,000.

Kanuni pia zinataka benki kupewa taarifa za kifedha zilizokaguliwa au notisi ya malipo ya gawio na ushahidi wa malipo ya kodi zote husika kabla ya kutuma fedha nje ya Tanzania inayohusiana na gawio au faida kwa wenye hisa wa kigeni. Mbaya zaidi, kanuni zimepiga marufuku wasiokuwa wakazi kununua, kuuza au kuhamisha dhamana za Serikali isipokuwa kwa eneo lililotajwa au kwenda kwa raia wa Tanzania katika jumuiya ya diaspora. Kwa upande wa mikopo kutoka nje, kanuni imeweka takwa linalotekelezwa chini ya Waraka juu ya Fedha za Kigeni, Na. 6000/DEN/EX.REG/58 wa Septemba 1998, kusajili mikopo kutoka nje inayovuka kipindi cha siku 365 na kupewa Namba ya Usajili wa Deni.

Mara baada ya kupokea mikopo /fedha kutoka nje na endapo mabenki yanashindwa kuwasilisha Benki Kuu ya Tanzania nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya usajili ndani ya siku 14, kanuni imetoa adhabu kwa benki kulipa TZS milioni 1 kwa kila siku ambayo mkopo unaendelea kutokuwa na

usajili. Kwa usawa, adhabu sawa na hiyo itatolewa kwa mkopaji endapo mkopaji anashindwa kuwasilisha benki nyaraka husika au mkopeshaji anatoa fedha za mkopo moja kwa moja kwa mgavi bila ya kuhusisha benki iliyosajiliwa nchini Tanzania na mkopo unaendelea kutokuwa na usajili kwa zaidi ya siku 14. Pia ni muhimu kufahamu kwamba Sheria zimepiga marufuku mabenki kusajili mikopo kutoka nje inayokiuka vigezo na masharti kama vile makubaliano yenye masharti ya awali yanayohitaji wakopaji kufungua akaunti ya fedha za kigeni nje ya Tanzania.

#### 4.3.5 Ulinganishi baina ya Tanzania na Nchi zilizochaguliwa katika Uimara wa Sarafu

Tanzania inashika nafasi ya 91st duniani. Nchi imeshuhudia kutotengemaa kwa fedha katika miaka iliyopita ikiwa na mfumuko mkubwa wa bei. Uimara wa sarafu ni kitu cha lazima kwa ukuaji. Vyote viwili; Serikali na makampuni ya biashara vinahitaji sarafu imara inayotumika kama njia ya kufanya biashara ili kupiga hatua katika ustawi na kufanya kazi kwa ufanisi. Hata hivyo, serikali bado inatumia vikwazo kwenye kumiliki fedha za kigeni na jambo hili linaweza kufanya maisha kuwa magumu kwa wafanyabiashara wa Tanzania wenye miradi yenye wigo wa kimataifa ambayo ndiyo aina sahihi kabisa ya biashara ambazo Tanzania inazihitaji ili kuinua uwezo zalishi na kutengeneza ustawi. Mfumuko wa bei hupoteza thamani ya ujira uliopatikana kihalali na akiba. Uimara wa sarafu, kwa maana hiyo, una umuhimu wa lazima katika kulinda haki ya kumiliki ardhi. Pale mfumuko wa bei unapokuwa siyo tu mkubwa bali unabadilika pia kwa haraka, inakuwa vigumu kwa watu kufanya mipango ya baadaye na kutumia kwa ufanisi uhuru wa kiuchumi. Vivyo hivyo, sehemu yenye umuhimu wa lazima ya uimara wa sarafu ni uwezo wa watu kununua na kumiliki sarafu za nchi nyingine.


Jedwali 4: Ulinganishi baina ya Tanzania na Nchi zilizochaguliwa katika Uimara wa Sarafu

| Na. | Nchi | Ukuaji wa fedha | S/D ya Mfumuko wa bei | Mfumuko wa bei (miaka ya hivi karibuni ) | Uhuru wa kumiliki akaunti ya benki katika fedha za kigeni | Uimara wa Sarafu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Japan | 9.48 | 9.82 | 10.00 | 10.00 | 9.82 |
| 2 | Albania | 9.78 | 9.69 | 9.68 | 10.00 | 9.79 |
| 3 | Costa Rica | 9.49 | 9.64 | 9.86 | 10.00 | 9.75 |
| 4 | Cape Verde | 9.40 | 9.59 | 9.88 | 10.00 | 9.72 |
| 5 | Denmark | 9.26 | 9.61 | 9.92 | 10.00 | 9.70 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Hong Kong | 9.12 | 9.54 | 9.95 | 10.00 | 9.65 |
| 7 | Marekani | 8.96 | 9.79 | 9.75 | 10.00 | 9.63 |
| 8 | Singapore | 9.28 | 9.24 | 9.96 | 10.00 | 9.62 |
| 9 | Uingereza | 9.21 | 9.40 | 9.80 | 10.00 | 9.60 |
| 10 | Nchi 10 za juu | 9.37 | 9.61 | 9.86 | 10.00 | 9.71 |
| 11 | Wastani wa Dunia | 8.41 | 8.50 | 8.87 | 7.18 | 8.24 |
| 12 | Botswana | 9.39 | 8.21 | 9.62 | 10.00 | 9.31 |
| 13 | Korea Kusini. | 9.24 | 9.48 | 9.89 | 10.00 | 9.65 |
| 14 | Afrika Mashariki | 8.39 | 7.67 | 8.63 | 8.33 | 8.26 |
| 15 | Kusini mwa Sahara | 8.12 | 8.22 | 8.45 | 4.67 | 7.36 |
| 16 | Tanzania | 10.00 | 9.03 | 9.34 | 5.00 | 8.34 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kielelezo 21: Uimara wa Sarafu




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

## 4.4 Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa

Biashara ni kiini cha ukuaji, Magai (2018) na kitu cha lazima kwa uhuru wa kiuchumi. Hii inaonekana hasa katika masoko ya kimataifa kutokana na kuimarika katika kujipambanua kwa sehemu mbalimbali za dunia. Uhuru wa kufanya biashara ni taratibu mbalimbali za kuondosha vikwazo vinavyoyumia ushuru na visivyotumia ushuru vinavyoathiri biashara ya kutoka nje na biashara ya nje ya bidhaa na huduma. Matokeo ya utafiti huu kutoka ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) yanaonesha kwamba kulikuwa na kiwango cha chini cha mabadiliko katika uhuru wa kufanya biashara ya kimataifa, mwaka 2015 kilikuwa 5.99, wakati ambapo mwaka 2016 kilikuwa 5.89, 2017 (5.96), na kwa upande mwingine mwaka 2019 kilikuwa 5.97. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba, kumekuwa na viwango vya chini vya mabadiliko katika uhuru wa kufanya biashara ya kimataifa, sehemu fulani kwa sababu utaratibu wa udhibiti unaosimamia biashara ya kimataifa umeendelea kutobadilika kati ya miaka hiyo ya 2016 na 2022

Kwa upande mwingine, kulikuwa na kiasi fulani cha mabadiliko katika kiwango cha ushuru. Matokeo ya utafiti huu utafiti katika Jedwali 5 yanaashiria kwamba mwaka 2015 kiwango kilikuwa 7.11, na 6.88 kwa mwaka 2016. Thamani ilishuka hadi 6.58 mwaka 2019. Kwa ujumla, mapato yatokanayo na kodi inayotozwa katika biashara yalishuka sana kutoka 8.82 mwaka 2015 hadi 7.34 mwaka 2019. Matokeo haya ya utafiti pia yanaashiria kwamba utaratibu wa udhibiti Tanzania haukubadilika kwa kiasi kikubwa kwa maana hiyo kupelekea ufanisi duni mwaka 2015 (2.98) na 2019(2.91) katika vikwazo vya kudhibiti biashara Kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka kwa viwango vya ushuru kiliendelea, kwa kiasi fulani, kubakia katika kiwango kilekile (5.1) kati ya 2015 hadi 2017, ikiwa na kiwango kidogo tu cha mabadiliko yaliyoonekana mwaka 2018 (5.06) na 2019 (5.02). Vikwazo vya biashara visivyotumia ushuru vilikuwa havitabiriki ambapo kiwango cha chini cha mwaka 2016 (4.82), wakati ambapo mwaka 2019 kilikuwa 5.03. Gharama za lazima za kuagiza bidhaa/huduma toka nje na kuuza nje bidhaa/huduma ziliendelea kuwa katika kiwango chake cha kutobadilikacha 0.80. Soko la biashara za magendo liliendelea bila ya kubadilika katika kipindi chote, hii ilikuwa hivyohivyo katika uhuru wa wageni kutembelea Tanzania.

Jedwali 5: Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa


| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa | 5.99 | 5.89 | 5.96 | 5.98 | 5.97 | 6.02 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A. Ushuru | 6.88 | 6.62 | 6.62 | 6.6 | 5.58 | 6.78 |
|  Mapato yatokanayo na kodi inayotozwa katika biashara (% ya sekta ya biashara) | 8.56 | 8.82 | 8.11 | 7.34 | 7.34 | 7.95 |
|  Wastani wa kiwango cha ushuru | 7.42 | 7.42 | 7.42 | 7.40 | 7.38 | 7.38 |
|  Kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka kwa viwango vya ushuru | 5.19 | 5.10 | 5.10 | 5.06 | 5.02 | 5.02 |
| B. Vikwazo vya kudhibiti biashara | 2.8 | 2.81 | 2.82 | 2.91 | 2.91 | 2.91 |
|  Vikwazo vya biashara visivyotumia ushuru | 5.16 | 4.82 | 4.85 | 5.03 | 5.03 | 5.02 |
|  Gharama ya lazima ya kuagiza bidhaa/huduma toka nje na kuuza nje bidhaa/huduma | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 |
| C. Viwango vya kubadilisha fedha soko la magendo | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 |
| D. Udhibiti wa uhamishaji wa mtaji na watu | 3.89 | 3.89 | 4.4 | 4.4 | 4.4 | 4.39 |
|  Uwazi Kifedha | 1.66 | 1.66 | 1.66 | 1.66 | 1.65 | 1.64 |
|  Udhibiti wa mtaji | 0 | 0 | 1.54 | 1.54 | 1.54 | 1.54 |
|  Uhuru wa wageni kutembelea | 10 | 10 | 10 | 10 | 10.0 | 10 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Tanzania bado inakabiliwa na gharama za juu zaidi za utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu na michakato ya taratibu za biashara inayopoteza muda mwingi sana ikilinganishwa nan chi nyingi miongoni mwa majirani zake wa eneo hilo. Utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu unamaanisha usimamizi mnyororo wa ugavi wa makampuni makubwa ambao ni kigezo kikuu cha kupima uwezo wao wa kushindana. Suala hili linahusiana na ufanisi na kuaminika kwa miundombinu ya usafiri, mamlaka za mpakani, wadhibiti usafiri, na watoa huduma. Kwa mfano, mwaka 2016, Tanzania ilishika nafasi ya 180 (kati ya nchi 189) katika urahisi wa kufanya biashara za kuvuka mipaka, ikisababishwa na ucheleweshaji mrefu na matakwa ya kujaza fomu nyingi. Nchi pia ilibakia katika kizio cha asilimia 80 kati yake nan chi zinazoongoza (mwenendo bora). Kwa maana hiyo, kuchochea ukuaji wawa sekta binafsi kunahitaji mazingira rafiki zaidi ya kufanya biashara.

Kielelezo 22: Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)


### 4.4.1 Kodi kwenye Biashara ya Kimataifa

Kwa mujibu wa ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021), uhuru wa kufanya biashara ya kimataifa, matokeo ya utafiti katika Kielelezo 22 yanaonesha kwamba ufanisi mwaka 2015 ulikuwa 5.99, 2016 tarakimu ya kiwango ilikuwa 5.89, wakati ambapo kulikuwa na kiwango kidogo sana cha mabadiliko 0.01 kati ya 2017, 2018 na 2019. Kwa mujibu wa Shirika la Fedha Duniani, Kodi kwenye biashara ya kimataifa (asilimia ya mapato) nchini Tanzania ilikuwa 6.74 kwa mwaka 2018, hii ilikuwa ongezeko kubwa kidogo ikilinganishwa na ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) ambapo tarakimu ya kiwango ilikuwa 5.98.

### 4.4.2 Wastani wa Kiwango cha ushuru

The wastani wa kiwango cha ushuru ni wastani wa ufanisi viwango vinavyotumika unaopimwa kwa mgao wa kuagiza bidhaa kwa kadri ya kila nchi mshirika. Kwa mujibu wa ripoti ya Taasisi ya Fraser, matokeo ya utafiti katika kielelezo12, wastani wa viwango vya ushuru mwaka 2015, 2016, na 2017 ulikuwa 7.42, hata hivyo, ulishuka kidogo hadi 7.4 mwaka 2018, na kidogo sana kwa 7.38 mwaka 2019 kama ulivyooneshwa katika Kielelezo 23.


Kielelezo 23: Wastani wa Viwango vya Ushuru




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kwa mujibu wa Ofisi ya Takwimu Tanzania viwango vya ushuru vilikuwa 6.62, 8.55, 8.37 na 8.9 kwa mwaka 2017, 2018, 2019, na 2020 mtawalia. Ndani ya miaka hiyohiyo, endapo utalinganisha na ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) kwa mfano mwaka 2017 kilikuwa 8.62, kwa upande mwingine ripoti ya Ofisi ya Takwimu Tanzania (2020) inaonesha kielezo cha 8.62.

Kielelezo 24: Viwango vya Ushuru Tanzania (2017-2020)




Chanzo: Ofisi ya Takwimu Tanzania (2022)

Viwango vya ushuru vinavyotumika katika ngazi ya kuzidisha kwa sita na nane hunafanya wastani wa bidhaa kwa kila kundi la bidhaa. Kwa mujibu wa Ofisi ya Takwimu Tanzania, viwango vya ushuru vilivyoorekodiwa kati ya 2015 na 2020 ni:-

- 2020 vilikuwa 8.94% kukiwa na ongezeko la 0.57% kutoka 2019

- 2019 vilikuwa 8.37% kukiwa na kushuka kwa 0.18% kutoka 2018
- 2018 vilikuwa 8.55% kukiwa na kushuka kwa 0.07% kutoka 2016.
- 2017 vilikuwa 8.62% kukiwa na ongezeko la 1.34% kutoka 2015.

#### 4.4.3 Kanuni ya Vikwazo vya Biashara

Kikwazo cha biashara ni kizuizi kilichowekwa na serikali katika mkondo wa kimataifa wa bidhaa au huduma. Mara nyingi huitwa "ulinzi" kwa sababu malengo yake their yaliyotajwa ni kukinga au kukuza viwanda au sehemu ya uchumi. Aina iliyozoeleka sana ya vikwazo vya kudhibiti biashara ni; zuio, ushuru (kodi kwenye bidhaa zinazotoka nje), na ruzuku ya serikali kwa sekta/viwanda fulani vya ndani.

Kadri nchi inavyokuwa na sheria nyingi zaidi za udhibiti ndivyo inavyokuwa na uelekeo mkubwa zaidi wa kuzuia biashara kuingia kwenye masoko na kupunguza uhuru wa kujihusisha sokoni, na kwa hiyo, kupunguza uhuru wa kiuchumi. Tathmini hizi huchunguza gharama za lazima za kuagiza bidhaa/huduma toka nje na kuuza nje bidhaa/huduma, Vikwazo visivyotumia ushuru na vikwazo vya kudhibiti biashara.

Jedwali 6: Sheria za Vikwazo vya biashara

| Miaka | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Vikwazo vya kudhibiti biashara | 2.98 | 2.81 | 2.82 | 2.91 | 2.91 | 2.91 |
| Vikwazo vya biashara visivyotumia ushuru | 5.16 | 4.82 | 4.85 | 5.03 | 5.03 | 5.03 |
| Viwango vya kubadilisha fedha soko la magendo | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 |
| Udhibiti wa uhamishaji wa mtaji na watu | 3.89 | 3.89 | 4.4 | 4.4 | 4.4 | 4.4 |
| Uwazi Kifedha | 1.66 | 1.66 | 1.66 | 1.66 | 1.65 | 1.65 |
| Udhibiti wa mtaji | 0 | 0 | 1.54 | 1.54 | 1.54 | 1.54 |
| Uhuru wa wageni kutembelea | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Matokeo ya utafiti katika Jedwali 6 yanaonesha mwelekeo wa Tanzania katika kielezi cha Vikwazo vya kudhibiti biashara kutoka kwenye Ripoti ya Taasisi ya Fraser. Ripoti zinaashiria kwamba, mwaka 2015 tarakimu ya kiwango ilikuwa 2.98, lakini mwaka 2016 tarakimu ya

kiwango ikawa 2.81, 2017 kiwango ilikuwa 9.82, wakati ilishuka hadi 9.16 mwaka 2018 na 2019. Kwa upande mwingine, Vikwazo visivyotumia ushuru vilikuwa katika kiwango cha 8.97 mwaka 2015; tarakimu ya kiwango haikubadilika (9.34) mwaka 2018 na 2019. Wakati huohuo, gharama ya lazima ya kuagiza bidhaa/huduma toka nje na kuuza nje bidhaa/huduma ilikuwa 8.88 mwaka 2015, iliongezeka hadi 8.97 mwaka 2016 kabla ya kushuka hadi 9.3. Kiwango cha mabadiliko kilichoripotiwa katika Kielelezo 21 kinaweza kuwa sababu ya mabadiliko ya duniani ya sera na kanuni zinazosimamia biashara ya kimataifa. Tanzania kuwa nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC inafuata utaratibu wa eneo hilo wa udhibiti wa bidhaa zinazotoka nje na biashara ya nje, na inafuata kanuni ya kimataifa ya asili kwa biashara ya bidhaa kutoka nje ya.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, Vikwazo visivyotumia ushuru vilivyowekwa rmpakani na karibu na mpaka huchangia katika gharama kubwa ya kufanya biashara Tanzania. Hivi vinajumuisha vikwazo vya kiufundi dhidi yakatika biashara, matakwa la kulinda afya ya binadamu, wanyama na mimea, taratibu za ushuru, kanuni za asili, biashara, na sheria za usafiri. Sheria zimehalalishwa kwa ajili ya kupata matokeo ya malengo ya sera ya serikali (afya, usalama, na ulinzi). Tatizo halipo katika msingi wa udhibiti ulio wa lazima. Hata hivyo, udhibiti wa lazima haupaswi kufikia hadi kushughulika na masuala ubora; haya hushughulikiwa vizuri zaidi kupitia viwango vya hiyari. Gharama kubwa za kufanya biashara kwa kiasi kikubwa husababishwa na njia ambayo udhibiti unatekelezwa. Taratibu zilizojaa usumbufu na zinazojirudiarudia, wasiwasi dhidi ya wafanyabiashara kutoka sekta binafsi, umuhimu wa mapato yanayotozwa rmpakani, vinavyoambatana na uwezo hafifu wa kiufundi na upungufu wa wafanyakazi huishia katika gharama kubwa za kufanya biashara.

Rahisisha na punguza idadi ya taasisi zinazohusika. Mwingiliano wa Mamlaka ya dawa na vifaa tiba awali ikijulikana kama mamlaka ya chakula na dawa umeshughulikiwa. Sasa, Shirika la Viwango Tanzania limepewa mamlaka ya kuidhinisha bidhaa zote za chakula na vipodozi ambazo awali zilihitaji kuthibitishwa na taasisi zote mbili za shirika la viwango na mamlaka ya chakula na dawa. Uamuzi wa serikali kusawazisha majukumu ya Shirika la Viwango Tanzania na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania una manufaa kadhaa kwa wafanyabiashara, idadi ya kibalivibali imepungua kutoka 4 hadi 1. Leo, wafanyabiashara siyo hawahitajiki kufanya maombi ya cheti cha usajili wa bidhaa; usajili wa jengo na biashara kibali kutoka mamlaka ya chakula na dawa (mf. Mamlaka ya dawa na vifaa tiba). Wafanya biashara hawahitajiki pia kulipa % 1.5ya thamani ya

FOB kwa ajili ya kupata kibali cha kuagiza bidhaa kutoka Mamlaka ya dawa na vifaa tiba. Kibali cha kuagiza bidhaa kinachotolewa na Mamlaka ya dawa na vifaa tiba kimefutwa.

Tanzania imechukua hatua kadhaa kutatua suala yanayohusiana na Vikwazo visivyotumia ushuru (NTB), kama vile Kituo Kimoja cha Huduma katika bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa Kituo Kimoja cha Huduma za Mpakani (OSBP); pia imeanzisha Mfumo wa Kielektronu wa Kufuatilia Mizigo(ETS) ili kurahisisha usimamizi wa malori yanayosafirisha mizigo kwenye nchi jirani. Iliamuliwa kuanzishwa mfumo wa kimtandao wa kutoa taarifa na usimamizi wa NTBunaofanywa na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) kupitia mfumo huo NTB vinaripotiwa na kufanyiwa tathmini kwa nia ya kuondolewa, japokuwa utekelezaji unasuasua

#### 4.4.4 Ulinganishi wa Nchi kwenye Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa

Kadri watu na wafanya biashara nchini Tanzania wanavyopaswa kuwa na uwezo wa kununua kutoka kwa mtu yeyote, na kuuza kwa mtu yeyote wanayependa katika taifa lao wenyewe, ndivyo wanavyopaswa kuwa na dunia yote kama sokoni kwao. Tanzania haiwezi kutengeneza ustawi na maisha bora zaidi kwa wananchi wake kwa msingi wasoko la watu milioni 60 wanaoishi katika taifa. Inahitaji watu wanaokaribia kufikia bilioni nane duniani kuwa soko lake. Tanzania inashika nafasi ya 112. Kiwango chake kimevuka kidogo wastani wa Afrika Mashariki na kusini mwa Sahara, lakini ipo nyuma sana ya mataifa yote yaliyofanikiwa katika sampuli badou ya kielelezo (Tazama Jedwali 7). Kiwango cha Tanzania na nafasi yake katika eneo hili kinapaswa kutoa hadhari kwa umma na watengenezaji wa sera kwa namna ileile. Vikwazo dhidi ya biashara Tanzania vimepelekea ukuaji uliosongwasongwa.

Jedwali 7: Ulinganishi baina ya Tanzania na Nchi zilizochaguliwa katika Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa

| nchi | Mapato ya kodi za biashara (% ya sekta ya biashara | Wastani wa Kiwango cha Ushuru | Kiasi kinachokubalika cha viwango vya ushuru | Ushuru | Vikwazo vya Biashara Visivyotumia Ushuru | Gharama za kutekeleza masharti ya kuagiza au kuuza bidhaa nje | Vikwazo vya kibiashara vya udhibiti | Viwango vya kubadilisha fedha katika soko la magendo | Udhibiti wa mtaji | Uhuru wa wageni kutembelea | Udhibiti wa kuhamisha mtaji na watu | Uhuru wa biashara kimataifa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Hong Kong | 10 | 10 | 10 | 10 | 8.32 | 9.67 | 8.99 | 10 | 7.69 | 0.11 | 5.93 | 8.73 |

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SAR, China | | | | | | | | | | | | |
| Singapore | 10 | 10 | 10 | 10 | 8.36 | 9.20 | 8.78 | 10 | 6.92 | 0.00 | 5.64 | 8.61 |
| Uholanzi | 8.60 | 8.98 | 6.51 | 8.03 | 7.15 | 9.98 | 8.56 | 10 | 8.46 | 5.00 | 7.82 | 8.60 |
| Romania | 8.60 | 8.98 | 6.51 | 8.03 | 6.26 | 9.97 | 8.11 | 10 | 8.46 | 5.00 | 7.82 | 8.49 |
| Denmark | 8.60 | 8.98 | 6.51 | 8.03 | 6.70 | 9.98 | 8.34 | 10 | 6.92 | 5.00 | 7.31 | 8.42 |
| Malta | 8.60 | 8.98 | 6.51 | 8.03 | 7.05 | 8.92 | 7.98 | 10 | 7.69 | 5.00 | 7.57 | 8.40 |
| Latvia | 8.60 | 8.98 | 6.51 | 8.03 | 6.76 | 9.42 | 8.09 | 10 | 6.92 | 5.00 | 7.31 | 8.36 |
| Estonia | 8.60 | 8.98 | 6.51 | 8.03 | 7.02 | 9.94 | 8.48 | 10 | 5.38 | 5.00 | 6.80 | 8.33 |
| Lithuania | 8.60 | 8.98 | 6.51 | 8.03 | 6.16 | 9.78 | 7.97 | 10 | 6.92 | 5.00 | 7.31 | 8.33 |
| Georgia | 9.89 | 9.72 | 8.71 | 9.44 | 6.50 | 9.58 | 8.04 | 10 | 6.92 | 0.00 | 5.64 | 8.28 |
| Nchi 10 za juu | 9.01 | 9.26 | 7.43 | 8.57 | 7.03 | 9.64 | 8.34 | 10 | 7.23 | 3.51 | 6.92 | 8.45 |
| Wastani wa Dunia | 8.31 | 8.16 | 5.89 | 7.41 | 5.66 | 6.54 | 6.10 | 9.46 | 3.59 | 1.46 | 3.49 | 6.62 |
| Botswana | 3.00 | 8.46 | 5.53 | 5.66 | 5.32 | 9.40 | 7.36 | 10 | 5.38 | 0.00 | 5.13 | 7.04 |
| Cape Verde | 7.64 | 7.96 | 4.74 | 6.78 | 5.11 | 6.66 | 5.88 | 10 | 9.23 | 0.00 | 6.01 | 7.17 |
| Korea Kusini. | 9.65 | 7.28 | 0.00 | 5.64 | 5.63 | 9.58 | 7.60 | 10 | 6.15 | 0.00 | 5.38 | 7.16 |
| Afrika Mashariki | 7.99 | 7.45 | 5.36 | 6.93 | 5.22 | 2.96 | 4.09 | 8.62 | 4.10 | 1.67 | 3.47 | 5.78 |
| Kusini mwa Sahara | 7.23 | 7.45 | 5.94 | 6.87 | 5.13 | 4.19 | 4.67 | 9.43 | 3.00 | 0.67 | 2.41 | 5.84 |
| Tanzania | 7.95 | 7.38 | 5.02 | 6.78 | 5.03 | 0.80 | 2.91 | 10.00 | 1.54 | 10.00 | 4.39 | 6.02 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Biashara inachechemea kwa urasimu, gharama za lazima, na vikwazo vya kudhibiti biashara. Tanzania ina viwango vibaya sana katika gharama za lazima, chini ya moja kati ya 10. Hii inamaanisha waagizaji wa bidhaa toka nje na wauzaji wa bidhaa nje ya Tanzania wanakabiliwa na gharama za urasimu unaodhoofisha. Jambo hili pia huchochea rushwa kwani inawapa maofisa fursa kutoa upendeleo kwa minajili ya kupokea rushwa.

Kiwango cha chini cha Tanzania katika vikwazo vya kudhibiti biashara kinaonyesha kwamba kuna vikwazo vikali, fursa nyingine ya rushwa. Vikwazo kwenye mtaji na uwekezaji kutoka nje ni kikwazo kwa uwekezaji kutoka nje unaoweza kutengeneza ajira na ustawi. Kiwango cha chini katika kiasi kinachokubalika cha kupanda na kushuka kwa ushuru kinaashiria kwamba serikali inajaribu kutoa upendeleo kwa baadhi ya sekta kuliko nyingine, badala ya kuruhusu uvumbuzi na uwezo wa makampuni kuonesha njia. Kwa bahati mbaya, baada ya maboresho fulani katika eneo la uwazi katika biashara nchini Tanzania, kiwango cha Tanzania kimeshuka zaidi katika miaka ya kuanzia 2010.

## 4.5 Sheria

Kimsingi mfumo wa udhibiti unalenga kusimamiana kuratibu shughuli za kiuchumi chini ya uchumi wa soko huria. Kipekee, kusahihisha hali ya kushindwa kwa nguvu za soko na kulinda usalama wa wanunuzi. Katika utekelezaji wa jambo hili, serikali imeasisi idadi kadhaa ya mamlaka za udhibiti. Kwa mfano, Tume ya Ushindani (FCC) ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa chuni ya Seksheni ya 62 (1) ya Sheria ya Ushindani, Na. 8 ya mwaka 2003 (FCA) kwa lengo la kuchochea na kulinda ushindani wenye tija katika biashara na kulinda wanunuzi dhidi ya mwenendo potofu wa soko na usio wa haki. Shabaha ya mbali ikiwa ni kuongeza ufanisi katika uzalishaji, mgawanyo na ugavi wa bidhaa na huduma.

Nchini Tanzania, kanuni kadhaa za udhibiti husimamiwa na mamlaka za udhibiti, baadhi yake ikijumuisha; Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA), Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mamlaka ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA), Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) Mamlaka Ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) nk. Mamlaka zote hizi hudai tozo mbalimbali na ada kwa maendeleo ya yao ya gharama za uendeshaji. Hizi tozo huongeza gharama ya kufanya biashara nchini Tanzania.

Jedwali 8: Udhibiti

| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kanuni | 6.32 | 6.62 | 6.27 | 6.68 | 6.71 | 7.03 |
| Udhibiti wa Soko la Mikopo | 7.82 | 8.18 | 7.84 | 8.18 | 8.19 | 8.44 |
| Umiliki wa Mabenki | 8 | 8 | 8 | 8 | 8 | 8.0 |
| Mikopo ya Sekta Binafsi | 8.37 | 8.27 | 8.27 | 8.27 | 8.27 | 8.31 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Udhibiti wa Kiwango cha Riba | 10 | 10 | 10 | 9 | 9 | 9.0 |
| Udhibiti wa Soko la Nguvukazi | 5.75 | 5.73 | 5.73 | 5.76 | 5.76 | 6.60 |
| Kanuni za kuajiri na kima cha chini cha mshahara | 5.57 | 5.57 | 5.57 | 5.57 | 5.57 | 5.57 |
| Kanuni za kuajiri na kuachisha kazi | 4.55 | 4.28 | 4.38 | 4.82 | 4.82 | 4.82 |
| Mawasiliano ya pamoja ya waajiri | 6.38 | 5.96 | 5.85 | 5.95 | 5.95 | 5.95 |
| Udhibiti wa muda wa kazi | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 |
| Gharama ya kuachishwa kazi | 8.27 | 8.27 | 8.27 | 8.27 | 8.27 | 8.27 |
| Kutumikia jeshi kwa mujibu wa sheria | 5 | 5 | 5 | 5 | 5.0 | 5.0 |
| Udhibiti wa Biashara | 5.65 | 5.93 | 5.22 | 6.09 | 6.20 | 6.04 |
| Mzigo wa usimamizi | 4.2 | 4.24 | 4.38 | 4.61 | 4.61 | 4.61 |
| Mzigo wa udhibiti | 2.44 | 1.78 | 2.0 | 1.56 | 1.56 | 1.33 |
| Kuanzisha biashara | 8.94 | 8.85 | 8.5 | 8.63 | 8.63 | 8.63 |
| Malipo ya ziada/rushwa/upendeleo | 5.97 | 5.93 | 5.32 | 6.10 | 6.10 | 6.10 |
| Kikwazo cha Leseni | 7.57 | 7.91 | 7.91 | 7.91 | 7.91 | 7.91 |
| Gharama za ulipaji wa kodi | 7.81 | 7.68 | 6.10 | 7.68 | 7.68 | 7.68 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)


### 4.5.1 Udhibiti wa Soko la Mikopo

Udhibiti wa soko la mikopo unajumuisha masuala kama; umiliki wa mabenki, mikopo ya sekta binafsi, udhibiti wa kiwango cha riba (kiwango hasi cha riba halisi). Katika masharti ya mikopo, Tanzania ni nchi ya 58. Hii inamaanisha kwamba wafanyabiashara na wajasiriamali wanapitia ugumu usio wa lazima katika kupata mikopo kwa ajili yakuanzisha au kutanua biashara na kutengeneza ajira na ustawi. Tanzania ilishika nafasi ya 13 kati ya nchi 15 kutoka Afrika kusimi mwa Sahara katika urahisi wa kupata mikopo. Kama soko linaloibuka, miradi mingi ya kibiashara nchini Tanzania imehangaika na uwezekano mgumu wa kupata mikopo, na asilimia 70 ya biashara zote za kati na ndogo nchini Tanzania, hazina uwezekano rasmi wa kupata mikopo kabisa. Kwa kweli, ni asilimia 15 tu ya watu wote ndio wenye uwezekano rasmi wa kupata mikopo kupitia mabenki.

Ukosefu wa mikopo haumaanishi kwamba Watanzania siyo wakopaji wa fedha, kwa kuwa zaidi ya nusu ya wale waliopo katika soko la nguvukazi wamewahi kuchukua mikopo wakati fulani.

Watanzania wengi wanatumia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi kama vile M-Pesa (ya Vodacom), Airtel Fedha (ya Airtel) na Tigo Pesa (ya Millicom), miongoni mwa mifumo mingine kupitia simu za mkononi fedha malipo inayotolewa na waendeshaji wa mtandao wa simu za mkononi (Mfumo usio wa kibenki) wakati ambapo watu wachache zaidi wana akaunti za benki katika mabenki yanayondesha shughuli zao nchini Tanzania (Mfumo wa kibenki). Idadi ya akaunti zilizosajiliwa na zinazotumika kwa huduma ya fedha kupitia simu za mkononi zilikuwa milioni 29.4 mwishoni mwa Desemba 2020, ikilinganishwa na milioni 24.4 na milioni 27.2 mwishoni mwa Desemba 2019 na Juni 2020, mtawalia.

Kielelezo 25: Udhibiti wa Soko la Mikopo




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Uchanganuzi wa ufanisi kupitia Taasisi ya Fraser umeashiria kwamba, kiwango cha udhibiti wa soko la mikopo mwaka 2017 kilikuwa 7.84. Kiliongezeka kwa 0.32 mwaka 2018 hadi 8.18, kiwango kilibaki katika ufanisi wake uleule mwaka 2019. Kiwango kinaonekana hivyo kwa sasa. Kufuatia janga la korona, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kuchukua mlolongo wa hatua za kisera kuitegemeza sekta ya kibenki, ikiwemo kushusha kiwangocha cini cha riba kutoka 7.0% hadi 5.0% na kupunguza kiwango cha chini cha uwiano wa mali na hifadhi kutoka 7.0% hadi 6.0% rasmi kuanzia 8 Juni 2020, ili kuchochea kuimarika kwa ufanisi wa soko.

Benki Kuu ya Tanzania kwa kiasi kikubwa imejikita kwenye kufanya usimamizi wa kibenki kwa uangalifu zaidi na kuchochea tasnia madhubuti ili kukuza uimara na ufanisi katika uendeshaji wake. Licha ya mdororo wa dunia katika mikopo ya kifedha na ukuaji mwaka 2020 kutokana na

UVIKO-19, sekta ya kibenki nchini Tanzania ilieindelea kuimarika katika kiwango cha 4.1% kwa mwaka. Huduma za kibenki kwa njia ya kidijitali zinaendelea kutanuka zikichochewa na kukua kwa ujumuishwaji wa kiuchumi na kiwango cha kuenea kwa matumizi ya simu za mkononi. Mwezi Mei 2020, Benki Kuu ya Tanzania iliongeza ukomo wa kila siku wa miamala kwa wateja wa mitandao ya simu za mkononi kutoka TZS milioni 3.0 hadi TZS milioni 5.0 na la kila siku salio la kila siku kutoka TZS milioni 5.0 hadi TZS milioni 10.0 ili kuchochea matumizi ya miamala ya huduma za malipo kwa njia ya mtandao wa simu na intaneti. Uwezo wa kompyuta kubadilishana taarifa katika huduma ya fedha kupitia simu za mkononi umechangia pia kwenye ukuaji wa jumla wa wa miamala fedha kupitia simu za mkononi wa 6.9% katika thamani ya muamala. Hata hivyo, kwa mwezi Aprili 2018, Serikali ya Tanzania imetengeneza mpango mpya wakuboresha mikopo kutoka sekta binafsi na kupunguza wingi wa mikopo mibaya. Kama inavyokadiriwa katika kielelezo.23 kuhusuana na udhibiti wa soko la mikopo, matokeo ya utafiti yanaonesha kumekuwa na kushuka kwa ufanisi wa udhibiti wa soko la mikopo, hii kwa sehemu fulani ilisababishwa na kutungwa kwa Sheria ya fedha kwa watu wa kipato cha chini na bunge mwaka 2018. Ilionesha mwaka 2017 kwamba karibia 48.6% ya watu nchini Tanzania walihudumiwa na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayotoa huduma za fedha, huduma ya fedha kupitia simu za mkononi, na taasisi nyingine kama vile vyama vya kuweka na kukopa, Mikopo endelevu na taasisi ndogo za kifedha.


Kanuni mpya zinawataka wote wanaotoa huduma za fedha kwa watu wa kipato cha chini kuwa na anuani sahihi inayotegemea ambayo ni sharti kuidhinishwa na ya Benki Kuu ya Tanzania, kwa kuongezea, mtoa huduma hawezi kufungua au kufunga sehemu ya biashara bila ya idhini ya Benki Kuu ya Tanzania iliyotolewa awali, kushindwa kutimiza masharti itakuwa ni kosa linalopelekea adhabu. Taasisi ndogo za kifedha pia inahitaji kutekeleza Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu na kutunza mahesabu yao kwa sahihi kulingana na viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa, ambayo yanapaswa kukaguliwa na mkaguzi wa mahesabu aliyesajiliwa na inawapasa kuwasilisha Benki Kuu ya Tanzania taarifa zao za fedha kwa mwaka. Kanuni hizi ziliishia kwa idadi ya taasisi ndogo za kifedha kufunga biashara kwa sababu ya kushindwa masharti

### 4.5.2 Udhibiti wa Kiwango cha Riba

Matokeo ya utafiti huu utafiti katika Jedwali 5 yameonesha ufanisi wa Tanzania katika udhibiti wa kiwango cha riba (viwango hasi vya riba halisi). Kielelezo kinaonyesha kwamba Tanzania

iliweza kudhibiti riba kwa kiwango kisichobadilika kutoka 2015 hadi 2017 kwa ufanisi wa 10; kiasi kikibadilika kati ya 2018 na 2019 hadi ufanisi wa 9. Viwango vya riba vinavyotozwa katika mikopo ya mabenki viliendelea kwa kufuata sera jumuishi ya fedha na hatua zilizotumika, ijapokuwa taratibu sana.

Kielelezo 26: Udhibiti wa Viwango vya Riba




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Kwa sasa vya jumla viwango vya riba za mikopo have vipo katika wastani wa 16.30%, ukishuka kutoka 16.37% na 16.63% katika uliotangulia na Januari 2021, mtawalia. Viwango vya riba za mikopo kwa maafikiano vilishuka hadi 13.68% kutoka 14.06% katika mwezi uliotangulia (Benki Kuu ya Tanzania, 2021 ripoti ya robo mwaka). Pia kuna haja ya kudokeza kwamba baadhi ya mabenki yalishusha viwango vya riba hadi digiti moja, hasa kwa upande wa kilimo.

Kwa mujibu wa kikokotoo cha Benki Kuu ya Tanzania, Viwango vya riba za mikopo na akiba kwa ujumla vilikuwa chini mwezi Juni 2019 na 2018, kuliko mwezi Juni 2018. Viwango vya jumla na viwango vya riba za mikopo kwa mwaka mmoja vilishuka kwa kipimo cha msingi cha 66 na kipimo cha msingi cha 1.25 mwaka hadi mwaka hadi kufikia wastani wa asilimia 16.84 na asilimia 16.36 mwezi Juni 2019, mtawalia. Hali hili inaakisi mwendelezo wa maboresho katika marasilimali ubora za benki na mchakato wa kutoa mkopo. Vivyo hivyo, cha jumla kiwango cha riba ya akiba kilishuka kwa kipimo cha msingi cha 52 hadi kufikia wastani wa asilimia 7.67. Hata

hivyo, kiwango cha riba ya akiba kwa miezi 12 kilipanda hadi kufikia wastani wa asilimia 9.22 mwezi Juni 2019 kutoka asilimia 8.68 mwezi Juni 2018.

Hata hivyo, kufuatia matokeo ya Janga la Uviko-19, mataifa tofauti kote duniani yalichukua hatua tofauti kushughulika na hali ya kiuchumi. Benki Kuu ya Tanzania ilichukua hatua kupunguza idadi ya Mikopo inayosuasua. Hii ilipelekea kusuasua katika ukuaji wa sekta binafsi na ongezeko la idadi ya Mikopo inayosuasua (Clyde na wenzake (Machi, 2018). Benki Kuu ya Tanzania ilipendekeza mikakati ya kiwango cha chini na kutoa misamaha ili kusaidia katika kushughulikia kuongezeka kwa idadi ya mikopo inayosuasua kupitia Waraka wa Benki Kuu ya Tanzania Na. FA.178/461/01/02. Matokeo yaya waraka ilikuwa ushahidi kwamba mikopo hiyo inayosuasua ilishuka kutoka asilimia 11.1 mwezi Aprili 2019 hadihadi asilimia 10.7 mwezi Juni 2019 na asilimia 9.8 mwezi Desemba 2019.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha unabainisha kwamba uwiano baina ya mikopo inayosuasua na jumla ya mikopo yote ya mabenki kwa wateja umeongezeka hadi asilimia 11 mwezi Aprili 2020 kufuatia mlipuko wa UVIKO-19. Hii hatua ilikusudiwa kuilinda uchumi kufuatia athari za UVIKO-19 na kupunguza hatari ya kudorora kwa mikopo yote iliyotolewa na mabenki kwa wateja. Hatua mbalimbali za kisera zilizobuniwa na Benki Kuu ya Tanzania zinajumuisha; kushusha hifadhikiwango cha chini cha matakwa ya uwiano wa mali, na kushusha viwango vya chini vya riba pamoja na mnyumbuliko katika udhibiti wa utoaji wa mikopo.


### 4.5.3 Udhibiti wa Soko la Nguvukazi

Udhibiti wa soko la nguvukazi unaweza kupelekea ubishani hasa. Uingiliaji kati wa serikali kama vile kutunga kanuni za usalama wa ajira na sheria za kima cha chini cha mshahara siyo tu unaonesha tofauti za kimtazamo kuhusu jukumu la Serikali na makubaliano ya wazi kati ya wanajamii kuhusu mtaji na nguvukazi, lakini una athari ya moja kwa moja kwenye riziki za watu. Tanzania inashika nafasi ya 79 katika udhibiti wa nguvukazi. Hii inamaanisha kuna vikwazo vikali katika soko la nguvukazi. Vikwazo hivi zaidihasa huwazuia watu maskini zaidi katika jamii wanapojaribu kutafuta ajira rasmi, hivyo inaongeza mivutano ya kijamii.

Mwishoni, kunakuwa na changamoto ya kuwa na mizania sawa kati ya kuwezesha mazingira bora ya kufanya kazi na vipato kwa waajiriwa na kuwapa waajiri mnyumbuliko wa kuendesha shughuli zao za kibiashara kwa ufanisi na kwa gharama inayostahili. Wakati ambapo siasa haiwezi kuwekwa kando, uchanganuzi makini utokanao na data unaweza kuchangia katika mchakato wa sera kwa kuonesha athari zinazoweza kusababishwa na chaguzi tofauti za udhibiti

kwenye matokeo muhimu ya kijamii na wa kiuchumi. Hii inajumuisha masuala kama; kanuni za kuajiri, kima cha chini cha mshahara, kuajiri na kuachisha watu kazi, mawasiliano ya pamoja ya waajiri, sheria ya muda wa kufanya kazi, gharama ya kuachishwa kazi, na Kutumikia jeshi kwa mujibu wa sheria.

Kielelezo 27: Udhibiti wa Soko la Nguvukazi




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)


Katika nchi ya kipato cha chini kama Tanzania, kwa kutumia mifano miwili tu, zaidi ya asilimia 80 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi ama wamejiajiri wenyewe au hujihusisha katika miradi ya familia. Katika muktadha huu, kanuni za usalama wa ajira, sheria za kima cha chini cha mshahara, na kanuni nyinginezo haziwezi kutumika kwa ufanisi sana. Jambo jingine ni kwamba, hata katika muundo mzuri zaidi wa masoko la nguvukazi ya nchi zinazoendeleza, masharti ya kodi ni changamoto ya kutisha. Waajiri ambao wangependa kuepuka gharama za kutimiza masharti ya kanuni za nguvukazi na waajiriwa ambao wanaopendelea kuongeza hadi upeo kipato cha kurudi nacho nyumbani wanaweza kirahisi tu kufanya kazi "kinyemela". Kwa mfano, katika idadi kubwa ya nchi zinazoendelea, kati ya robo na nusu ya watu wanaopokea ujira hulipwa pungufu ya kima cha chini cha mshahara. Wakazi wanafurahia kiasi fulani cha uhuru wa msingi unaofungamana na kusafiri na kubadili eneo la makazi, ajira, na elimu hasa wale wanaotoka katika Nchi Wanachama

wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati ambapo Itifaki ya Soko la Pamoja, inayohusisha uhamishaji huru wa nguvukazi, inatekelezwa ingawa siyo kikamilifu.

### 4.5.4 Udhibiti wa biashara

Taifa linaloshika nafasi ya 127 katika udhibiti wa biashara lipo katika nafasi mbaya sana. Vizuizi vinavyodhibiti uanzishaji na upanuzi wa wa biashara ni mzigo mzito katika ukuaji wa biashara na utengenezaji wa ajira nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Ripoti ya Taasisi ya Fraiser (2021), kuna idadi ya masuala ambayo ndiyo msingi wa ripoti, yanayojumuisha; mzigo wa usimamizi, kuanzisha biashara, malipo ya ziada/rushwa/upendeleo, vikwazo katika Utoaji wa Leseni, na Gharama ya Ulipaji wa kodi. Kuna kanuni kadhaa za udhibiti wa biashara zenye kawaida ya kukwamisha ufanisi wa biashara nchini Tanzania. Baadhi ya changamoto ni:- uwepo wa gharama kubwa za lazima kwa muktadha wa kifedha na muda katika suanzishaji na uendeshaji wa biashara; taratibu za uidhinishaji wa awali zilizojaa usumbufu, ambazo hutoa fursa za michezo ya hila; kuwepo kwa michakato mingi inayojirudia; mianya inayosababisha hasara katika sbaadhi ya sheria na kanuni zinazotumiwa na wadhibiti wakati wa kufanya ukaguzi; na gharama kubwa za utekelezaji wa kanuni.

Kielelezo 28: Udhibiti wa biashara




Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Matokeo ya utafiti katika kielelezo hapo juu yameonesha kwamba kulikuwa na kiasi kikubwa cha maboresho mazingira ya biashara Tanzania. Kwa mfano mwaka 2017 kiwango kilikuwa 5.22, ufanisi uliongezeka kwa 0.31, ongezeko hili lilipelekea kiwango cha 6.09 mwaka 2018, na 6.2 mwaka 2019. Uchanganuzi wa kimaandishi umeweka wazi kwamba, serikali imejaribu kuchukua hatua kadhaa na kufanya mageuzi kwa ajili ya kushughulikia changamoto zinazokabili mwenendo wa biashara nchini Tanzania. Baadhi ya mageuzi haya ni; kuanzishwa kwa Mfumo wa Pamoja wa Forodha Tanzania (TANCIS), uliotengenezwa katika misingi wa teknolojia ya juu kwa dhamira ya kuongeza ufanisi, tija, uwazi, na kuaminika katika usimamizi wa ushuru; serikali imeanzisha pia Mfumo wa Dirisha Moja la Malipo (ESWS). Haya mageuzi mawili yanalenga kuwezesha mazingira yanayohusiana ya biashara katika kituo kimoja cha huduma kinachohitaji mamlaka za udhibiti wa biashara kuratibu shughuli zao kwa namna itakayoepusha wafanyabiashara kufanya malipo/miamala mingi inayojirudia.

### 4.5.5 Ulinganishi baina ya Tanzania na Nchi zilizochaguliwa katika Biashara Udhibiti

Udhibiti mkali kupita kiasi unaweza kuvuruga uanzishwaji wa biashara mpya, kukatisha tamaa upanuzi wa biashara, na kupunguza faida, mambo ambayo ndiyo njia ya kuchochea na kutoa hamasa kwa uwekezaji zaidi. Tanzania inashika nafasi ya 127 katika udhibiti wa biashara, ikiwa na maana kwamba urasimu uliokithiri unauzonga uwezo wa biashara kutengeneza ajira na ustawi. Changamoto chache ni muhimu zaidi kwa Tanzania kuliko utengenezaji wa ajira na kwa hiyo inahitaji kufanya biashara yake kuwa huru ili kutengeneza ajira.

Jedwali 9: Ulinganishi baina ya Tanzania na Nchi zilizochaguliwa katika Udhibiti wa biashara

| Nchi | matakwa ya usimamizi | gharama za Urasimu | Kuanzisha biashara | Malipo ya ziada, rushwa, upendeleo | vikwazo katika utoaji wa leseni | Ulipaji wa kodi | Udhibiti wa biashara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Singapore | 7.44 | 9.78 | 9.95 | 8.76 | 9.99 | 9.28 | 9.20 |
| Estonia | 5.20 | 8.89 | 9.83 | 9.65 | 9.24 | 9.44 | 8.71 |
| Finland | 6.49 | 7.56 | 9.56 | 8.93 | 9.86 | 8.99 | 8.56 |
| New Zealand | 5.19 | 8.44 | 9.98 | 9.65 | 9.40 | 8.43 | 8.52 |
| Taiwan | 4.90 | 9.56 | 9.66 | 9.27 | 9.58 | 7.52 | 8.42 |
| Hong | 7.31 | 8.44 | 9.95 | 5.00 | 9.79 | 9.61 | 8.35 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kong | | | | | | | |
| Uswisi | 6.32 | 6.22 | 9.58 | 9.79 | 8.37 | 9.29 | 8.26 |
| Australia | 3.98 | 8.00 | 9.93 | 9.64 | 8.95 | 8.82 | 8.22 |
| Japan | 5.01 | 8.44 | 9.56 | 8.18 | 9.15 | 8.56 | 8.15 |
| Georgia | 6.08 | 7.78 | 9.95 | 7.50 | 9.89 | 7.58 | 8.13 |
| Nchi 10 za juu | 5.79 | 8.31 | 9.79 | 8.64 | 9.42 | 8.75 | 8.45 |
| Wastani wa Dunia | 4.15 | 5.08 | 9.19 | 5.67 | 8.39 | 7.35 | 6.63 |
| Botswana | 4.15 | 6.67 | 8.46 | 8.28 | 9.26 | 8.65 | 7.58 |
| Cape Verde | 4.53 | 6.44 | 9.58 | 6.40 | 9.27 | 7.98 | 7.37 |
| Korea Kusini. | 3.76 | 9.11 | 9.59 | 7.88 | 9.99 | 8.05 | 8.06 |
| Afrika Mashariki | 4.69 | 3.30 | 9.27 | 4.75 | 8.88 | 7.66 | 6.43 |
| Kusini mwa Sahara | 4.02 | 3.71 | 8.98 | 5.01 | 8.46 | 6.92 | 6.15 |
| Tanzania | 4.61 | 1.33 | 8.63 | 6.10 | 7.91 | 7.68 | 6.04 |

Chanzo: ripoti ya Taasisi ya Fraser (2022)

Tanzania ipo nyuma katika maeneo yote mawili ya Afrika Mashariki na kusini mwa Sahara na hata nyuma zaidi ya wastani wa dunia. Mambo yote mawili; matakwa ya wasimamizi na urasimu huzorotesha uanzishwaji wa biashara na kudhoofisha biashara zilizopo. Ukiwa wa gharama ya juu, ulipaji wa kodi unatumia muda wa wamiliki wa biashara wakati ambapo wanapaswa kujikita kujenga na kukuza biashara zao. Biashara inalazimika kukidhi gharama za ulipaji wa kodi na bado serikali haipati mapato. Kuondolewa kwa mlolongo huu mnene wa urasimu uliokithiri kutamaliza tatizo jingine kubwa, malipo ya ziada. Matakwa mazito ya wasimamizi na gharama ya urasimu hupelekea rushwa kwa sababu ya kutoa mwanya kwa maofisa kuomba rushwa kwa minajili ya kupata njia ya mkato dhidi ya urasimu uliokithiri. Mara nyingi urasimu kufungua fursa for rushwa kwa makusudi hutengeneza urasimu na ucheleweshaji uliokithiri.

Tanzania iliwahi kuwa na viwango vya chini kupindukia katika eneo hili na Tanzania imeendelea kudorora katika kiwango cha udhibiti wa biashara.

# 5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Hitimisho

Mkazo wa utafiti huu ulikuwa ni kuchanganua ripoti ya Taasisi ya Fraser iliyotolewa hivi karibuni ya "Orodha ya Nchi kwa Viwango vya Uhuru wa Kiuchumi Duniani", na kufanya uchanganuzi kuchunguza "Kiwango cha Uboreshaji wa Uhuru wa Kiuchumi Tanzania 2021". Kipekee, utafiti huu ulishughulikia malengo yafuatayo; lengo la kwanza lilikuwa ni kuhakiki na kufanya uchunguzi wa kitaifa juu ya "Uhuru wa Kiuchumi nchini Tanzania 2021" kulingana na mapengo yaliyobainika. Lengo la pili lilikuwa ni kuhakiki tafiti nyingine za ndani na kimataifa, kuendesha majadiliano ya mashauriano, mahojiano, na majadiliano ya vikundi lengwa juu ya mada husika kulingana na mapengo yaliyobainika. Lengo la tatu lilikuwa ni kupendekeza Mageuzi ya Sera katika maeneo manne kama vile Mfumo wa Kisheria na Haki ya Kumiliki Ardhi, Uimara wa Sarafu, Uhuru wa Kufanya Biashara ya Kimataifa na Udhibiti kwa ajili ya kuingizwa katika Michakato ya Utayarishaji wa Sera nchini Tanzania. Lengo la nne lilikuwa ni kutoa ripoti ya Viwango vya Uhuru wa Kiuchumi nchini Tanzania vilivyo bora zaidi na mapendekezo ya sera kwa ajili ya kuwasilishwa kwa watunga sera.

Uchanganuzi wa ripoti ya Taasisi ya Fraser (2021) unaonesha kwamba taasisi zinazojitegemea katika Nchi huwa na athari chanya katika ukuaji wa kiuchumi. Kupitia ulinzi wa haki ya kumiliki ardhi, kuondoa rushwa pamoja na kupunguza matokeo ya misukumo hasi ya nje, inayozorotesha ukuaji wa kiuchumi. Sera zisizofaa zina kawaida ya kusababisha anguko katika ukuaji wa kiuchumi hadi chini ya uwezekano wake. Kufuatia kuchanganuliwa uhuru wa kiuchumi Tanzania, pamoja na uhusiano wake na ukuaji wa kiuchumi, hoja zifuatazo za kuhitimisha zimefikiwa katika maeneo yafuatayo; uhuru wa kiuchumi unapishana kwa kiasi kikubwa katika vielezi vinne ambavyo utafiti huu ulipima; Ikilinganishwa na mataifa mengine, Nchi zenye uhuru zaidi wa kiuchumi hukua haraka zaidina kufikia viwango vya juu zaidi vya kipato kwa mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo, kuna uhusiano chanya baina ya mabadiliko katika uhuru wa kiuchumi na ukuaji wa kipato kwa mtu mmoja mmoja; Uhuru wa kiuchumi unawiana kwa karibu sana na ustawi wa jumla wa jamii; Nchi zilizo huru zaidi kiuchumi zinayapita mataifa yenye uhuru hafifu kama viashiria vya ustawi wa jamii. Pia ilionesha, uhuru wa kiuchumi na utawala unaozingatia sheria husaidia kuchangia katika ukuaji wa kiuchumi. Tanzania imepiga hatua katika kuwa huru zaidi. Kuasisiwa kwa Makubaliano ya Biashara Huria kwa kupunguza, na baadaye, kutokomeza

vikwazo vya biashara na ushuru umepelekea Tanzania na nchi nyingine katika eneo la SADC kuwa huru zaidi kiuchumi kwa minajili ya biashara ya kimataifa.

Vielezi vya uhuru vya Taasisi ya Fraser vinaripoti kwamba Tanzania, kama nchi nyingine za SADC na ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa takriban asilimia 7 nyuma ya wastani wa dunia katika uhuru wa kufanya biashara.

Mfumuko wa bei na uimara bei vinaonekana kuwa katika viwango vibaya zaidi tangu mwanzoni mwa muongo. Hata hivyo, kumekuwa na maendeleo chanya toka mwaka 2015 hadi 2019. Hii inaashiria kwamba wakati Tanzania kama inavyolinganishwa na nchi nyingine katika eneo la SADC imepiga hatua katika kuwa huru zaidi, katika upande wa uhuru wa fedha na uhuru wa kumiliki fedha za kigeni. Kigezo cha uhuru wa fedha ni takriban asilimia 3 chini ya wastani wa dunia. Mgogoro wa hivi karibuni wa kifedha na kiuchumi umepelekea nchi nyingi ikiwemo Tanzania kusitisha misimamo yao katika uhuru wa kiuchumi. Jambo hili litaendeleza tu mdororo wa kiuchumi na kudhoofisha ukuaji wa kiuchumi. Hata hivyo, chaguzi sahihi za sera zitalinda maendeleo katika uhuru wa kiuchumi, na kuruhusu ukuaji wa kiuchumi kutokea. Kiwango cha jumla katika orodha ya uhuru duniani kilishuka kwakwa pointi 0.1.

Uhuru wa jumla wa kiuchumi Tanzania katika vielezi vinne kama ilivyochunguzwa katika utafiti huu kutoka 2015 hadi 2019 umeonesha ongezeko kwa pointi 0.1. Hii ni dalili ya wazi kwamba nchi inapiga hatua katika kuwa huru zaidi na matokeo yake, kuinua ukuaji wake wa kiuchumi. Kinadharia, uhuru wa kiuchumi unahakikisha kuwa na matokeo mazuri kwenye ukuaji wa kiuchumi, na kuashiria kwamba matokeo yauhuru wa kiuchumi imara kwa kiasi kikubwa zaidi kuliko yale ya uwazi. Uhuru wa kiuchumi una jukumu muhimu katika ukuaji wa kiuchumi. Ushahidi wa kinadharia ulionesha pia uhusiano wa moja kwa moja kati ya uhuru wa kiuchumi na ukuaji wa kiuchumi. Inaweza kuhitimishwa kwamba Tanzania imeongeza nafasi yake ukuaji wa kiuchumi kwa kuwa huru zaidi, lakini haina maana uhuru utaongezeka zaidi kwa kuinua ukuaji wa kiuchumi.

## 5.2 Mapendekezo

(i) Uelewa uliopatikana kupitia machapisho umeashiria kwamba uhuru wa kiuchumi hupelekea ukuaji wa kiuchumi na ustawi wa jamii. Hapana budi kuchukua hatua ili kufikia viashiria vya msingi vya uhuru wa kiuchumi.

(ii) Hali ya kuteleza iliyoonekana katika mwenendo kuhusiana na mfumo wa kisheria na haki ya kumiliki ardhi inastahili kutazamwa kwa umakini. Marekebisho yaliyofanyika kwenye

sheria mbalimbali yaliyoshusha haki ya kumiliki ardhi au kupelekea kushuka kwa uhuru katika mfumo wa mahakama yanastahili kupitiwa upya kutokana na uzoefu uliopatikana hadi sasa.

(iii) Changamoto za utekelezaji wa haki ya wanawake kumiliki ardhi hazina budi kushughulikiwa kwa ukuzaji wa kiwango cha uelewa wa sheria hizi na uimarishaji wa mbinu za utekelezaji na kufanya uhakiki wa sheria kandamizi za mila, mazoea, desturi za urithi, mila na desturi zinazowanyima wanawake haki ya kumiliki ardhi.

(iv) Kumekuwa na kiwango cha chini cha mabadiliko katika uhuru wa kufanya biashara ya kimataifa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015-2019 lakini huu mwelekeo chanya umeharibiwa na kushuka kodi inayotozwa katika biashara ikiashiria kwamba vikwazo vya kudhibiti biashara havina budi kulegezwa. Kwa maana hiyo, kuinua kiwango cha mawasiliano, ikiwemo kushirikishana taarifa kati ya mamlaka zote zinazohusika katika uondoaji wa mizigo mpakani, kutapunguza gharama ya biashara rmpakani. Kuhakikisha kwamba pande zote tayari wana uwezo wa kupata taarifa sahihi kuhusiana na sheria na michakato ya usimamizi inayohitajika kwa ajili ya kuagiza bidhaa/huduma toka nje na kuuza nje bidhaa/huduma kupitia Kituo cha Taifa cha Habari za Biashara inaweza kupunguza ucheleweshaji wa gharama wa uondoaji wa mizigo. Kurahisisha na kuondoa mizengwe mipakani na sera ya udhibiti mipakani kutaongeza mapato na kupunguza biashara.

(v) Tanzania haina budi kuendelea taratibu za ushuru katika uondoaji wa mizigo kuwa za kisasa ili kushughulikia gharama za ugavi na usafirishaji na urahisi wa kufanya biashara, hii inayohitaji utekelezaji wa Mfumo wa Dirisha Moja la Malipo na kupitisha Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki juu ya Kituo Kimoja cha Huduma Mpakani. Maboresho katika usimamizi wa kielektroniki wa data na mchakato wa kielektroniki vitawezesha Tanzania kuongeza matumizi ya utayari wa kushughulika na hatari na taswira ya hatari.

(vi) TRA kuendelea kuanzisha mageuzi ya kuwezesha biashara, ikiwemo kuongezeka kwa imani katika utayari wa kushughulika na hatari kama nyenzo ya kudhibiti idadi ya kaguzi zinazofanyika kwa gharama ya juu. Zaidi, ushirikiano wa kikanda ni msingi katika kupunguza gharama ya biashara. Uzoefu utokanao na Kituo Kimoja cha Huduma Mpakani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki unaashiria kwamba majengo na vitendea kazi pamoja na mageuzi muhimu ya kitaasisi na kikanuni ni msingi wa kushuka kwa muda unaotumika kuvuka mpaka.

(vii) Benki Kuu ya Tanzania haina budi kuongeza kasi ya kufanya usimamizi wa kibenki kwa uangalifu zaidi na kuchochea tasnia madhubuti kukuza uimara wake na ufanisi katika uendeshaji wake. Sera ya fedha ya benki kuu haina budi kusaidia ukuaji wa huduma za kidijitali za kibenki kwa ajili ya kuendelea kutanua huduma za kifedha kwa njia ya mtandao wa simu na intaneti, ujumuishwaji wa kiuchumi na boresha mikopo kutoka sekta binafsi wakati huohuo kupunguza idadi ya mikopo inayosuasua.

(viii) Udhibiti wa soko la nguvukazi hauna budi kushughulikia taswira kubwa ya mizania sawa kati ya kuwezesha mazingira bora ya kufanya kazi na vipato kwa waajiriwa na kuwapa waajiri mnyumbuliko wa kuendesha shughuli zao za kibiashara kwa ufanisi na kwa gharama inayostahili.

(ix) Punguza vikwazo vya biashara vinavyozuia uwezo wa kuyafikia masoko ya biashara ya nje. Kazi kuu ni kurahisisha na kuondoa mizengwe katika upatikanaji wa vibali vya biashara ili kupunguza mzigo wa udhibiti kwa biashara ndogo na wafanyabiashara wadogo. Wakati ambapo kanuni kutumika kwa makampuni yote, matokeo yake yanapishana na hasa yanakuwa mzigo mzito kwa makampuni madogo. Makampuni makubwa na yale ya kimataifa hunufaika na uzalishaji wao mkubwa wa gharama nafuu na huajiri wafanyakazi wa kutimiza masharti mengi ya udhibiti. Vivyo hivyo, gharama za ukaguzi hazina manufaa ya kiuchumi kwa biashara ndogo.

(x) Imarishwa uwezo wa kitaasisi, masuala makuu matatu yanayohitaji kushughulikiwa ni; kukuza stadi za wafanyakazi na kudumu nao kwa muda wa kutosha kwenye nafasi zenye uhitaji mkubwa wa kiufundi; kupata zana za kutosha za majaribio na usimamizi mzuri wa vitendea kazi; na mawasiliano bora zaidi baina ya taasisi na taasisi, kwa kuwa kuna idadi kubwa ya mamlaka zinazohusika katika Hatua za udhibiti zisizotumia ushuru. Kupitia utekelezaji wa shughuli Tume za Kitaifa za Uwezeshaji wa Biashara na Kuondolewa kwa Vikwazo visivyotumia ushuru zinazojumuisha wajumbe kutoka sekta ya umma na binafsi, masuala hayo yamezingatiwa.

(xi) Imarishwa mfumo wa Malipo mtandao ili kushughulika na tatizo la malipo yasiyo rasmi na kuepuka mianya ya rushwa kwa watumishi wa umma wasiokuwa waaminifu. Kwa sasa Taasisi tofauti zimeanzisha mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma. Hizi zinajumuisha; Matumizi ya mtandao wa intaneti katika Usajili wa Makampuni, Majina ya biashara, usajili wa Biashara na huduma Nembo, haki Bunifu na usajili wa Leseni za Viwanda; Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia Simu za Mkononi (GePG), Mfumo wa faili

mtandao, Mfumo wa Uhamiaji Mtandaoni (e-Immigration). Wakati ambapo malipo yote yanayohusiana na Mamlaka za Serikali hulipwa kupitia namba maalumu ya malipo.

(xii) Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja, inayohusisha uhamishaji huru wa nguvukazi, hauna budi kuharakishwa na maendeleo yake kufanyiwa tathmini kwa kuzingatia uhuru wa msingi unaofungamana na kusafiri na kubadili eneo la makazi katika eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki, ajira, na elimu ya asilikwa wanaotoka katika Nchi Wanachama wa ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(xiii) Hapana budi kuchukua hatua ili kukuza mazingira ya udhibiti yenye uwezo wa kuchochea ushindani mkubwa zaidi katika biashara kwa msingi wa kutoa shuduma kwa kusawazisha hali katika eneo hili kwa dhamira ya kufanya tozo kuwa za ushindani zaidi.

(xiv) Masharti ya uhuru wa wadhibiti harakati ya kuchukua hatua zinazostahili kutoa ulinzi dhidi ya kujiingiza kwa kauli za kisiasa zilizo kinyume na uhuru na zinazotolewa kwa wadhibiti chini ya sheria.

(xv) Mageuzi mengine yanayohitajika ni:-

- Mafunzo ya kina juu ya mahakama ili kukuza uelewa wa umma juu ya uhuru na uwajibikaji ili kuleta uelewa kwa watengenezaji wa sera kuhusu kiasi cha madaraka yao juu ya majaji na Idara ya mahakama.
- Weka kiashiria cha wazi cha sifa za majaji na mahakimu, isiyokuwa na namna yoyote ya kujiingiza kwa upendeleo wa serikali na undugu.
- Unda bodi/kamati maadili ya kimahakama itakayosimamiwa na mamlaka ya mahakama. Hii inapaswa kujumuisha mamlaka ya mahakama kutengeneza bajeti na kusimamia fedha zake, matumizi, na uwezo wa kukutana na washirika wa maendeleo bila ya ulazima wa kufuata utaratibu wa kirasimu ndani ya the serikali.
- Fanya ununuzi na ufungaji wa mifumo inayojiendesha (kujaza fomu, kuchukua kumbukumbu za mwenendo, kufuatilia maendeleo yake nk).
- Unda Chombo cha Kitaifa cha Urasmishaji (NAB), kwa kuwekeza kazika vitendea kazi vyenye ubora, na kuboresha urasmishaji wa vitendea kazi vyenye ubora.
- Sawazisha sheria zinazotumika Zanzibar na zinazotumika Tanzania Bara, na kufanyia kazi kwa the kutambuliwa kimataifa kwa kanuni zinazotumika Zanzibar.

- Ongeza mawasiliano kati ya taasisi za Serikali na sekta binafsi kupitia mpango wa PPD, wa kukuza uelewa juu ya udhibiti na maarifa mengine kwa kufanya Kituo cha Taifa cha Habari za Biashara kuwa cha kisasa.
- Ongeza idadi ya rasilimali-watu yenye ustadi katika mamlaka za umma ili kuimarishwa Ari ya uvumbuzi, Utafiti na Maendeleo.
- Tumia kikamilifu Kituo cha Maelezo cha Taifa (NEP) kwa ajili ya kupata taarifa zinazohusiana na viwango na udhibiti wa kiufundi katika bidhaa/huduma nchi za nje ili wenye viwanda na wafanyabiashara wapate taarifa mapema kabla ya kufanya biashara ya nje.
- TIRA kuanzisha huduma ya mikopo ya Boma kukidhi hatari za zinazoweza kupindukia matakwa ya 5% kwa ajili ya mabenki kupata msamaha kutoka Benki Kuu ya Tanzania.
- Sawazisha uzani kwa ekseli unaotumika Jumuiya ya Afrika Mashariki na uzani kwa ekseli wa SADC kwa madhumuni ya kufanya wasafirishaji wa Tanzania kuwa shindani zaidi kwa wasafirishaji kutoka eneo la SADC. Kwa sasa, Malori ya Tanzania yanabeba 1.5 pungufu ikilinganishwa na wenzao wa SADC, ikiongeza 5% zaidi katika gharama ya usafirishaji.

## REJEA


Barry Wood (2008). ” Uhuru wa Kiuchumi Unapokuwa Thabiti, Kiwango 14 cha Uhuru wa Kiuchumi Kinaonesha”. Makavazi, 2008.

BEACH, William W. & KANE, Tim (2007) Mbinu: Upimaji wa Nchi 10 katika Uhuru wa Kiuchumi, 2007 Kiwango cha Uhuru wa Kiuchumi, Heritage Foundation, na Washington, D.C. Bennett, D., & Nikolaev, B. (2017). Uhusiano tata usio na usawa katika uhuru wa kiuchumi. Empirical Economics, 53(2), 717–754.

Carl J. Schramm (15 Januari 2008). "Sura ya 1 Ugiligili wa Kiuchumi: Kipimo Muhimu cha Uhuru wa Kiuchumi. Marekebisho ya 4 Februari 2008.

Edwin J. Feulner (2012). Hatua Moja Nyuma katika Uhuru wa Kiuchumi mwaka 2012. Jarida la Wall Street. Marekebisho ya, 2012. Feldmann, H. (2017). Uhuru wa kiuchumi na uwekezaji katika mtaji-watu. Jarida la Taasisi ya Kiuchumi,13(2), 421–445. Graafland, J., & Lous, B. (2018). Uhuru wa kiuchumi, hali ya kutokuwa sawa katika kipato na inhale ya kuridhika na maisha katika nchi za OECD. Jarida la Masomo ya Furaha,19, 2071–2093. Gwartney, J., Hall, J., & Lawson, R. (2017). Uhuru wa kiuchumi wa dunia: taarifa ya mwaka 2017. Marekebisho ya, 2018,

KANE, Tim (2007) Uhuru wa Kiuchumi katika Kanda Tano, 2007 Kiwango cha Uhuru wa Kiuchumi, Heritage Foundation, Dow Jones & Company, Inc., Washington, D.C., 57-72.

Magai, P.S., (2018): Uchanganuzi wa Kiuchumi wa Biashara na Ukuaji wa Kiuchumi nchini Tanzania: Ushahidi kutoka Data za Vipindi vya Nyakati. Jarida la Uhakiki wa Usimamizi wa Biashara, Vol 21 (1), pp. 74-84.

Noor Kapdi na Robert Parring (2018) gazeti. www.Dentons.Com

Palmer, R. 1999. “Sheria ya Ardhi Tanzania, 1999: Uchanganuzi wa Wachanganuzi,” http://www.oxfam.org.uk/landrights, Oxfam, Oxford.

Shivji, I.G. 1999. “Sheria ya Ardhi 1999: Sababu ya Sherehe au Sherehe ya Sababu?” Hotuba ya Msingi katika Warsha juu ya Ardhi, iliyofanyika Morogoro 19-20 Februari 1999.

Issa Shivji: Upembuzi wa Mahaba na Hofu dhidi ya Magufuli katika Jarida la CODESRIA. Mtandaoni. Namba 13. Juni 21.

Dawson, John W. (1998). Taasisi, Uwekezaji, na Ukuaji: Ushahidi Mpya wa Kukatambuga na Data za Jopo. Maulizo ya Kiuchumi 36 (October): 603-19.

De Haan, J., na J-E. Sturm (2000). Juu ya Uhusiano baina ya Uhuru wa Kiuchumi na Ukuaji wa Kiuchumi. jarida la Ulaya la Siasa ya Uchumu 16: 215–41.

Farr, W. Ken, Richard A. Lord, na J. Larry Wolfenbarger (1998). "Uhuru wa Kiuchumi, Uhuru wa Kisiasa na Ustawi wa Kiuchumi: Uchanganuzi wa Visababishi." Jarida la Cato 18, 2 (Fall): 247–62.

Fike, Rosemarie (2017). "Marekebisho ya Hali ya Kutokuwa Sawa Kijinsia katika Uhuru wa Kiuchumi na Kwanini ni Muhimu" kwa Gwartney, Lawson, na Hall, 2017. Taasisi ya Fraser: Vancouver.

Griswold, Daniel T. (2004). Kuchuuza Uonevu kwa Uhuru: Jinsi Masoko Huria Yalivyopalilia Ardhi ya Demokrasia. Taasisi ya Cato: Washington, DC. Uchanganuzi wa Sera ya Biashara No. 26, Januari 6.

Grubel, Herbert G. (1998). "Uhuru wa Kiuchumi na Ustawi wa Watu: Baadhi ya Tafiti Muhimu." Jarida la Cato 18, 2 (Fall): 287–304.

Karabegović, Amela na Jason Clemens (2005). Ukomeshaji wa Ajira za Watoto—Marufuku siyo Utatuzi. Kongamano la Fraser (Marhi).

Gwartney, James, Randall Holcombe, na Robert Lawson (1998). "Wigo wa Serikali na Utajiri wa Mataifa." Jarida la Cato 18, 2 (Fall): 163–90.

Gwartney, James, Robert Lawson na Walter Block (1996). Uhuru wa Kiuchumi wa dunia: Taarifa ya mwaka 1996. Vancouver: Taasisi ya Fraser.

Gwartney, James, na Robert Lawson (2004). Uhuru wa Kiuchumi wa dunia: 2004 Taarifa ya mwaka. Taasisi ya Fraser. <http://www.freetheworld.com>.

Gwartney, James, Robert Lawson na Joshua Hall, (2014). Uhuru wa Kiuchumi wa dunia: Taarifa ya mwaka 2014. Vancouver: Taasisi ya Fraser.

Gwartney, James, Robert Lawson na Joshua Hall, (2017). Uhuru wa Kiuchumi wa dunia: Taarifa ya mwaka 2017. Vancouver: Taasisi ya Fraser.

Gwartney, James, Robert Lawson, Joshua Hall na Ryan Murphy, (2022). Uhuru wa Kiuchumi wa dunia: Taarifa ya mwaka 2022. Vancouver: Taasisi ya Fraser.

Hall, Joshua, na Robert Lawson (2014). Uhuru wa Kiuchumi wa dunia: Sera ya Uchumi wa Kisasa 32, 1: 1–19. <http:// http://onlinelibrary.wiley.com/doi/10.1111/coep.2014.32.issue-1/issuetoc>.

Norton, Seth W., na James. D. Gwartney (2008). Uhuru wa Kiuchumi na Umaskini wa Dunia. Katika James Gwartney na Robert Lawson, Uhuru wa Kiuchumi wa dunia: 2008 Taarifa ya mwaka (Taasisi ya Fraser: 2008): 23–40.

Sala-i-Martin, Xavier. 2002. "Ongezeko Linalotatiza la Hali ya Kutokuwa Sawa katika Kipato Duniani". Kimechapishwa na JEL na kinapatikana kupitia: http://www.columbia.edu/~xs23/papers/GlobalIncomeInequality.htm, iliyotumika Julai 19, 2014.